DAWAT-E-ISLAMI

نیکی کی دعوت (Swahili)

Mlango wa Faizan-e-Sunnat - juzuu ya 2



# دَعوةُ الخَيرِ

# DA'AWAH YA WEMA


Sheikh-e-Tariqat, Amir-e-Ahl-e-Sunnat
Muasisi wa Dawat-e-Islami, Allamah Maulana Abu Bilal

**MUHAMMAD ILYAS**

**Attar Qadiri Razavi** دامت برکاتہم العالیہ

نَیکی کی دَعوَت

Nayki ki Da'wat

# *Da'awah ya wema*

## *(wito kwa wema)*

### *Mlango wa Faizan-e-Sunnat - juzuu ya 2*

Shaykh-e-Tareeqat, Ameer-e-Ahl-e-Sunnat,
Mwanzilishi wa Dawat-e-Islami, 'Allamah Maulana Abu Bilal

Muhammad Ilyas Attar

دَامَتْ بَرَكَاتُهُمُ الْعَالِيَه

◈

*Imetafsiriwa kwa Kiingereza / Kiswahili na*

Translation Department (Dawat-e-Islami)

# Wito kwa wema / Da’wah ya wema

Tafsiri ya  Kiswahili ya ‘Nayki ki Da’wat’

◆

**HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA**

Hakimiliki © 2024 Maktaba-tul-Madinah

Hairuhusiwi kunakili, kuhifadhiwa katika mfumo wa urejeshaji au kusambazwa, kwa namna yoyote au kwa njia yoyote ile, kielektroniki, mitambo, kunakili, kurekodiwa au vinginevyo, bila ya idhini ya maandishi ya Maktaba-tul-Madinah.

| | | |
|---|---|---|
| **Chapisho la** | : | Shaban-ul-Mu’azzam, 1445 AH (February, 2024) |
| **Imetafsiriwa na** | : | Translation Department (Dawat-e-Islami) |
| **Mchapishaji** | : | Maktaba-tul-Madinah |
| **ISBN** | : | 978-969-631-827-9 |
| **Kiasi** | : | - |

## UFADHILI

Tafadhali jisikie huru kuwasiliana nasi ikiwa ungependa kufadhili uchapishaji wa kitabu cha kidini au kijitabu kwa ajili ya Isal-e-Sawab ya wanafamilia wako waliofariki.

**Maktaba-tul-Madinah**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah – Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi,
Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

**E-mail:** maktabaglobal@dawateislami.net – maktaba@dawateislami.net

**Simu:** +92-21-34921389-93

**Mtandao:** www.dawateislami.net

# *Yaliyomo kwa Muhtasari*

Jedwali la kina la yaliyomo linaweza kuonekana mwishoni mwa kitabu.


| | | |
|---|---|---|
| 1. | Du’a ya Kusoma Kitabu. | iv |
| 2. | Dibaji | v-viii |
| 3. | Nia ishirini na tatu ya Kusoma Kitabu hiki | ix-x |
| 4. | Vidokezo vya Mtafsiri | xi |
| 5. | Hoja za (mambo muhimu ya ) Kukumbuka xii | xii |
| 6. | **Haja ya Wito (Da’awah) kwa wema** | **1-113** |

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ
اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

# *Du'a ya Kusoma Kitabu*

Soma Du'a (Dua) ifuatayo kabla ya kusoma kitabu cha dini au somo la Kiislamu, utakumbuka chochote unachosoma, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ:

اَللّٰهُمَّ افْتَحْ عَلَيْنَا حِكْمَتَكَ وَانْشُرْ
عَلَيْنَا رَحْمَتَكَ يَا ذَاالْجَلَالِ وَالْاِكْرَام

*Tafsiri*

*Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ Utufungulie milango ya elimu na hekima, na uturehemu, Ewe Ambaye ni Mwenye utukufu na ni Mtukufu!*

*(Al-Mustatraf, juzuu ya 1, uk. 40)*

**Kumbuka:**

Soma Salat-'Alan-Nabiy ﷺ mara moja kabla na baada ya Du'a.

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ

اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

# Dibaji

Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Siku ya Kiyama, [watu wa] Ummah wangu watakuwa wengi zaidi kwa idadi kuliko wale wa Ambiya wengine wote. *(Sahih Muslim, uk. 128, Hadiyth 331)*

Akizungumzia juu ya Hadiyth iliyotajwa hapo juu, mfasiri mashuhuri, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Kutakuwa na safu mia moja na ishirini za watu wa Peponi ambao miongoni mwao safu themanini zitakuwa za ummah wa Mtume Muhammad Mustafa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, na safu arubaini (40) zitakuwa za ummah wa Ambiya wengine عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام. *(Sunan-ut-Tirmizi, juzuu ya 4, uk. 245, Hadees 2555)*

Mufti mtukufu رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema zaidi: Kama Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ni mtawala (mfalme ) wa mitume wengine wote ,Ummah wake vile vile ni mtawala wa Ummah zingine zote. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 8, uk. 585-586)*

Mamilioni ya shukrani kwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ Ambaye Ametuumba sisi wanadamu na Akatujaalia kuwa Waislamu kutoka katika Umma wa Rasuli Kipenzi Chake na Aliyebarikiwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Moja ya sababu za ukuu na utukufu, adhama na utakatifu, na kunyanyuliwa na kuinuliwa kwa Ummah huu duniani na Akhera na Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ni kuwa Ummah huu unatimiza amri ya ﴿اَمْرٌ بِالْمَعْرُوْف وَ نَهْيٌ عَنِ الْمُنْكَر﴾ *(yaani kuwasilisha wito wa wema na kuzuia maovu).*

Hapa kuna Aya ya 110 ya Surah Aal-e-'Imran, sehemu ya 4 pamoja na tafsiri yake kutoka ukurasa wa 129 wa *Kanz-ul-Iman* tukufu pamoja na *Khaza`in-ul-'Irfan* iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami. Amesema Allah عَزَّوَجَلَّ:

كُنْتُمْ خَيْرَ اُمَّةٍ اُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ تَاْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَ تَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ وَ تُؤْمِنُوْنَ بِاللّٰهِ ؕ

*Nyinyi ni mbora miongoni mwa walimwengu wote walio tokea kati ya watu - mnaamrisha mema na mnakataza maovu na mnamuamini Mwenyezi Mungu.*

*[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 4, Surah Aal-e-'Imran, Ayah 110)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Kila Mwislamu ni mhubiri – awe ni mwanachuoni au mwanafunzi, Imamu wa Msikiti au Muadhini, kiongozi wa kiroho au mfuasi, mfanya biashara au mteja, mwajiri au mwajiriwa, afisa au kibarua, mtawala au mtu wa kawaida - bila kujali cheo chake cha kitaaluma na kijamii, anapaswa kuendelea kukuza Sunnah, kufikisha 'wito wa wema' kwa watu anaoishi nao au kufanya kazi nao. Ajitahidi kutekeleza kazi hii kubwa kwa nia njema ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ akitumia uwezo wake vyema.

Kwa masikitiko makubwa, Waislamu wa leo wamekuwa wavivu sana katika kufanya shughuli hii ya Madani inayohitajika sana. Ili kubadilisha uvivu huu kuwa shauku, Dawat-e-Islami, vuguvugu la kidini la kimataifa la Quran na Sunnah, na lisilo la kisiasa, tayari limechukua hatua kadhaa za kweli kwa kuandaa Ijtima'aat yenye msukumo wa Sunnah, Madani Qafilah ,ziara ya eneo kufikisha mwito wa mema, kozi za kufundisha Tabia za Madani, kozi ya Fard 'Uloom, Idhaa ya Madani na Dars kutoka katika kitabu Faizan-e-Sunnat n.k. Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ sura tano za Faizan-e-Sunnat, yaani. (i) Baraka za ﴿بِسْمِ اللهِ﴾ (ii) Adabu za Kiislamu za Kula (iii) Ubora wa Njaa (iv) Baraka za Ramadhani na (v) Kusengenya – Saratani katika Jamii Yetu, hadi sasa zimetoka.

Mikononi mwako sasa kuna sura ya sita 'Wito wa Wema' ambayo ina ubora na fadhila za kufikisha 'wito wa wema' na hasara za kuiacha. (Hii ni sura kubwa sana. Nimekusudia kufanyia kazi mada nyingi kama vile mifano ya Ambiya عَلَيْهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام, kafara zilizotolewa na maswahaba waliobarikiwa kwa ajili ya 'wito wa wema', 'wito kwenye wema' kwa kutumia karama [Muujiza]. 'Da'awah kwa wema kwa kutumia barua, Da'awah ya wema baada ya kufa na wahubiri vijana n.k Mauti yanaweza kuja wakati wowote. Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ambariki na amlinde kipenzi changu Madani Majlis 'Al-Madina-tul-'Ilmiyyah! wasia yangu kwa Majlis hii ni kuendelea kuzifanyia kazi mada hizi hata baada ya kufariki kwangu, na kuzijumuisha katika Faizan-e-Sunnat).

Kitabu hiki kinajumuisha karibu Aya mia moja ishirini na tano za Qur'ani (125), misemo 249 ya Rasuli Mpenzi na Mwenye Baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mafumbo ya mawaidha mia moja kumi na tatu (113), mafumbo ya kimadani Hamsini na moja (51), na lulu

mamia za kimadani kuhusu mada mbalimbali . Kwa rehema za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ, natumai kwamba kitabu hiki kitazidisha hamasa ya ndugu na dada wa Kiislamu kwa ajili ya shughuli kubwa ya Madani ya 'kuita watu kwenye wema'. Tumefanya tuwezavyo ili kuondoa makosa kutoka kwa kitabu hiki. Mufti wa Dawat-e-Islami 'Dar-ul-Ifta Ahl-e-Sunnat' pia ameiangalia kwa mtazamo wa Shar'i. اَلْحَمْدُلِلّٰه عَزَّوَجَلَّ Mimi ni nyeti sana kuhusu makosa. napendelea vitabu vyangu na vijitabu vya Na'at vikaguliwe na wanavyuoni kabla ya kuchapishwa kwa kuhofia kwamba iwapo hukumu fulani mbaya itachapishwa na watu kuanza kuifanyia kazi, huenda nikawajibishwa kwa hilo katika Akhera. Hata hivyo, tumefanya tuwezavyo lakini uwezekano wa makosa bado hauwezi kuondolewa. Kwa hivyo, ukipata kosa lolote la Shari katika kitabu hiki, tafadhali nifahamishe kuhusu hilo kwa nia njema, na upate kustahiki malipo makubwa (thawabu). Sitabishana bila sababu kwa kupendelea maoni yangu lakini nitaachana nayo kwa shukrani,

## Ombi la 'Attar

Ni ombi langu la Madani kwa kaka na dada wa Kiislamu kutoa angalau Dars mbili (moja kati ya hizo iwe nyumbani) kwa nia njema ya kupata radhi za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. Yaani wasomee Waislamu sehemu za kitabu hiki kwa nyakati mbili tofauti. Iwapo mtu yeyote, akianza kufuata njia ya Qur'an na Sunnah baada ya kusikia Darasa yako, wewe pia utafaulu, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ. Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Ikiwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ Atambariki hata mtu mmoja kwa uwongofu kwa sababu yenu, hii ni bora kwenu kuliko kuwa na ngamia wekundu. *(Sahih Muslim uk. 1311 , Hadith 2406)*

Katika maelezo ya Hadiyth iliyotajwa hapo juu, 'Allamah Yahya Bin Sharaf Nawavi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Ngamia wekundu walikuwa wakichukuliwa kuwa ni mali ya thamani miongoni mwa Waarabu, na hivyo walitajwa hapa kuwa ni mfano. Hii ni kwa maelezo tu; vinginevyo, ukweli ni kwamba hata sehemu ndogo ya Akhera isiyo na mwisho ni bora kuliko ulimwengu usiohesabika wa wanadamu.'*(Sharh Muslim lin-Nawavi, juz. 15, uk. 178).*

## Du'a ya 'Attar

Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Yeyote anayesoma kitabu 'Da'awah kwa wema (sehemu ya 1)' kuanzia mwanzo hadi mwisho ndani ya siku 25 na kutoa au kusikiliza Dars mbili kila siku kutoka katika kitabu 'Faizan-e-Sunnat', mbariki kwa : uthabiti katika Iman, kwa

kumtazama Mpenzi na Mbarikiwa Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم wakati wa mateso ya kifo chake, kusoma Kalimah wakati wa kufa kwake, faraja katika kaburi lake na wakati wa kufufuliwa, msamaha bila ya hesabu kutoka kwa rehema yako, Jannat- ul – firdaus katika ujirani wa Kipenzi Chako Rasuli صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Naomba zijibiwe dua zote hizi kwa ajili yangu, wanachuoni, cheki na wale wote walioshirikiana katika kukikamilisha kitabu hiki, wakiwemo Wanigran na wajumbe wa Majlis Maktaba-tul-Madinah, na wafanyakazi wote wa Maktaba-tul-Madinah. Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Samehe Ummah yote.

*Hay Tujh say Du'a Rab-e-Rahmat, maqbool ho Faizan-e-Sunnat*

*Ghar ghar Masjid Masjid perh ker Islami bhai sunata rahay!*

*Tafsiri: Ni maombi yangu kwa Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema عَزَّوَجَلَّ kwamba 'Faizan-e-Sunnat' iwe maarufu duniani kote. Watu watoe Dars kutoka humo majumbani, Masajid n.k.!*

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب      صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

تُوْبُوْا اِلَى الله      اَسْتَغْفِرُ الله

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب      صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

**Muhammad Ilyas Attar Qaadiri**
2 Ramadhani-ul-Mubarak, 1432 AH (Agosti 3, 2011)

اَلۡحَمۡدُ لِلّٰہِ رَبِّ الۡعٰلَمِیۡنَ وَ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَامُ عَلٰی سَیِّدِ الۡمُرۡسَلِیۡنَ

اَمَّا بَعۡدُ فَاَعُوۡذُ بِاللّٰہِ مِنَ الشَّیۡطٰنِ الرَّجِیۡمِ ؕ بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ ؕ

# *Nia ishirini na tatu za kusoma kitabu hiki*

Mtume kwa wanadamu, amani ya mioyo yetu na akili zetu, mkarimu na mkarimu zaidi. صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema:

نِيَّةُ الْمُؤْمِنِ خَيْرٌ مِّنْ عَمَلِهٖ

*Nia ya Muislamu ni bora kuliko kitendo chake.*

*(Al-Mu'jam-ul-Kabeer, gombo la 6, uk. 185, Hadees 5942)*

## Lulu mbili za Madani:

- ❖ bila nia njema, hakuna malipo yanayotolewa kwa tendo jema.
- ❖ Kadiri mtu anavyokuwa na nia njema, ndivyo atakavyopata thawabu zaidi.

## Nia

Kila ninaposoma kitabu hiki, nitaanza kwa kukariri

1. Hamd.
2. Salat (kumswalia mtume)
3. Ta'awwuz na
4. Tasmiyah. (Mtu anaweza kuchukua hatua juu ya nia hizi zote nne kwa kusoma mistari ya Kiarabu iliyotolewa juu ya ukurasa huu).
5. Nitasoma kitabu hiki mwanzo hadi mwisho kwa ajili ya radhi za Allah عَزَّوَجَلَّ.
6. Kwa uwezo wangu wote, nitajaribu kuisoma katika hali ya Wudhu,
7. Nikikabili Qiblah.
8. Nitazitazama Ayah za Qur'ani,
9. na Hadithi zenye Baraka.

10. (huku nikisoma kitabu) kila nikisoma neno lililobarikiwa 'Allah', nitasema ﴿عَزَّوَجَلَّ﴾.

11. na kila nikisoma jina lililobarikiwa la Mpendwa na Mbarikiwa Rasool nitasoma ﴿صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم﴾.

12. Nitajifunza maamuzi ya Shar'i.

13. Ikiwa sikuweza kuelewa hukumu fulani, nitashauriana na wasomi.

14. Sayyiduna Sufyan bin 'Uyaynah رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: ﴿عِنْدَ ذِكْرِالصَّالِحِيْنَ تَنْزِلُ الرَّحْمَةُ﴾ Rehema inashuka wakati wa kutajwa kwa wachamungu. *(Hilyat-ul-Awliya, gombo la 7, uk. 335, Raqm 10750)* Nitavuna baraka za kutajwa kwa wachamungu kwa kuwaambia mifano ya watakatifu wachamungu kutoka katika kitabu hiki, kwa wengine.

15. (Kwenye nakala yangu ya kibinafsi) Nitasisitiza mambo muhimu na muhimu na vidokezo vya kuyaangazia.

16. Nitaandika mambo muhimu ninaposoma.

17. Ili kukisoma kitabu hicho kabisa kwa nia ya kupata elimu ya dini nitasoma baadhi ya kurasa kila siku na kupata thawabu (ya kupata elimu ya dini).

18. Nitawahamasisha wengine kusoma kitabu hiki.

19. Kwa nia ya kutenda juu ya Hadiyth: ﴿ تَهَادَوْا تَحَابُّوْا ﴾ peaneni zawadi, itaimarika mapenzi kati yenu. *(Muwatta Imam Maalik, juzuu ya 2, uk. 407, Raqm 1731)* Nitanunua (nakala moja au nyingi za kitabu hiki niwezavyo kumudu) na nitawapa wengine zawadi.

20. Baada ya kuwapa wengine zawadi, nitawauliza waweke lengo la kusoma kitabu hiki kabisa (kwa mfano - ndani ya siku 25).

21. Nitawafundisha wale wasiojua.

22. Nitafanya Isal-e-Sawab ya kusoma kitabu hiki kwa Ummah wote.

23. Nikipata kosa lolote la Shar'i, nitamfahamisha mchapishaji kuhusu kosa hilo kwa maandishi (kumjulisha mchapishaji na mwandishi kwa maneno kwa kawaida haifanyi kazi).

اَلۡحَمۡدُ لِلّٰہِ رَبِّ الۡعٰلَمِیۡنَ وَ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَامُ عَلٰی سَیِّدِ الۡمُرۡسَلِیۡنَ

اَمَّا بَعۡدُ فَاَعُوۡذُ بِاللّٰہِ مِنَ الشَّیۡطٰنِ الرَّجِیۡمِ ؕ بِسۡمِ اللّٰہِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ ؕ

## *Vidokezo vya Mfasiri*

Ndugu wapenzi wa kiislamu! Translation Department ya Dawat-e-Islami, idara inayohusika na utayarishaji wa vitabu na vijitabu vya Ameer-e-Ahl-e-Sunnat, mwanzilishi wa Dawat-e-Islami 'Allamah Maulana Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qaadiri Razavi دَامَتۡ بَرَکَاتُہُمُ الۡعَالِیَہ katika lugha mbalimbali za Ulimwengu, unafuraha kuwasilisha kitabu '*Nayki Ki Da'wat*' kwa Kiswahili kwa jina la '*da'awah kwa wema*'.

Ingawa tafsiri yoyote bila shaka ni aina ya ufafanuzi, tumejaribu kiwango chetu bora kuwasilisha wazo la mwandishi katika maana yake halisi. Masharti ya sheria ya Kiislamu hayajatafsiriwa kama tahadhari kwa sababu katika hali nyingi, neno la Kiswahili haliwezi kuwa mbadala kamili wa neno la Kiislamu. Hata hivyo, faharasa imetolewa mwishoni mwa kitabu, ikifafanua maneno ya Kiislamu. Kwa ajili ya urahisi wa kaka na dada wa Kiislamu ambao watakuwa wakitoa dars kutoka katika kitabu hiki, sura fupi yenye Ahadi thelathini kuhusu ubora wa Salat-'Alan-Nabii pia imeongezwa. Zaidi ya hayo, faharasa na katalogi pia zimetolewa.

Tafsiri hii imetimizwa kwa neema ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ, kwa neema ya Mtukufu Rasool صَلَّى اللهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم na msaada wa kiroho wa Shaykh wetu mkuu, mwanzilishi wa Dawat-e-Islami, 'Allamah Maulana Abu Bilal Muhammad Ilyas Attar Qaadiri Razavi دَامَتۡ بَرَکَاتُہُمُ الۡعَالِیَہ. Ukipata upungufu wowote katika kazi hii, inaweza kuwa hitilafu ya kibinadamu kwa upande wa tafsiri ya Majlis, na wala si mwandishi wa kitabu asili. Kwa hivyo, ukipata kosa lolote au upungufu katika kitabu hiki tafadhali tujulishe kulihusu kwa kuandika katika anwani ifuatayo ya posta au barua pepe kwa nia ya kupata thawabu (Sawab).

**Translation Department (Idara ya Tafsiri)**

Aalami Madani Markaz, Faizan-e-Madinah – Mahallah Saudagran, Purani Sabzi Mandi, Bab-ul-Madinah, Karachi, Pakistan

**UAN:** ☎ +92-21-111-25-26-92 – Ext. 7213

**Barua pepe:** 🖃 translation@dawateislami.net

# *Mambo ya kukumbuka*

Angazia mambo mbalimbali unaposoma kitabu inapobidi. Andika mada na uingize nambari ya ukurasa katika safu wima zilizo hapa chini. Maarifa yako yataimarishwa, اِنْ شَآءَاللّٰہ عَزَّوَجَلَّ.

| Mada | Kurasa | Mada | Kurasa |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

اَلْحَمْدُ لِلّٰهِ رَبِّ الْعٰلَمِيْنَ وَالصَّلٰوةُ وَالسَّلَامُ عَلٰى سَيِّدِ الْمُرْسَلِيْنَ

اَمَّا بَعْدُ فَاَعُوْذُ بِاللّٰهِ مِنَ الشَّيْطٰنِ الرَّجِيْمِ ؕ بِسْمِ اللّٰهِ الرَّحْمٰنِ الرَّحِيْمِ ؕ

# HAJA YA WITO KWA WEMA

## Ijtima' ya msamaha

Sayyiduna Abu Hurayrah رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُ amesimulia kwamba Rasuli mashuhuri na mwenye heshima صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم Amesema: Kuna malaika wa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ wanaotembea. Wanapopita kwenye makusanyiko ya Zikr, huambiana wao kwa wao, 'Keti (hapa)' Wanapofanya Du'a wale wanaofanya Zikr (katika mkusanyiko), Malaika hawa husema ﴿اٰمِيْن﴾ kwa Du'a yao. Wanaposoma Salat-'Alan-Nabiy, Malaika pia huswali pamoja nao. Wakati wanatawanyika [jitenga], Malaika huambiana wao kwa wao kwamba kuna habari njema kwa watu hawa waliobahatika,kuwa wanaporejea, wamesamehewa. *(Jam'-ul-Jawami' lis-Suyuti, juzuu ya 3, uk. 125, Hadiyth 7750)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Fadhila tatu za kuhudhuria Msikiti.

سُبْحٰنَ اللّٰہ عَزَّوَجَلَّ! Ni bora iliyoje mikusanyiko ya Zikr! Kumbuka kwamba Ijtima'aat, Dars na Ijtima'-e-Zikr-o-Na'at zenye msukumo wa Sunnah pia zinazingatiwa kuwa ni mikusanyiko ya Zikr. Wana bahati iliyoje Waislamu wanaohudhuria Ijtima'aat hizi za rehema kwa moyo wote, wakipata fursa ya kusamehewa kwa neema ya Mwenyezi Mungu! Hata hivyo, si kila mtu anayeweza kupata fursa ya kuhudhuria Ijtima'aat hizi za msamaha; waliobahatika tu ndio hubarikiwa nayo. Kwa vile ni tendo la wema sana na la kupata thawabu kuhudhuria vikao vya Madani vya Dars na hotuba zinazofanyika kwa kawaida huko Masajid, Shetani pia anajaribu sana kuwazuia watu kuhudhuria Msikiti. Anzisha 'kampeni ya kujaza Masjid'. Wahamasishe Waislamu kuhudhuria Masjid na hivyo kumfanya Shetani asifanikiwe.

Sayyiduna 'Abdur Rahman Bin Ma'qil رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُ amesema, 'Tumesikia (kutoka kwa wanachuoni) ﴿اَلْمَسْجِدُ حِصْنٌ حَصِيْنٌ مِّنَ الشَّيْطٰنِ﴾ yaani Masjid ni ngome imara ya kujikinga na Shetani. *(Musannaf Ibn Abi Shaybah, juzuu ya 8, uk. 172)*

Kwa ajili ya msukumo wako, hapa kuna maneno matatu ya Rasuli Mpenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kuhusu ubora wa Msikiti:

1. Bila shaka, wale wanaohudhuria na kuwafanya wengine kuhudhuria nyumba za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ hakika hao ndio waja wa kweli wa Mwenyezi Mungu. *(Al-Mu'jam-ul-Awsat, juzuu ya 2, uk. 58, Hadiyth 2502)*
2. Mwenye kuupenda Masjid Allah عَزَّوَجَلَّ humfanya kuwa kipenzi chake. *(Ibid, gombo la 4, uk. 400, Hadees 6383)*
3. Mja anapoendelea kukaa Msikitini kwa ajili ya Zikr au Swalah, Allah عَزَّوَجَلَّ humwonea huruma, kama watu wa familia ya yule aliyepotea hufurahi anaporudi. *(Sunan Ibn Majah, juzuu ya 1, uk. 438, Hadiyth 800)*

*Woh salamat raha Qiyamat mayn*
*Perh liye jis nay dil say chaar salam*

*Mayray Piyaray kulipa mayray Aqa kwa*
*Mayri janib sema laki bar salam*

*Mayri bigri bananay walay per*
*Bhayj ay mayray Kirdgar salam*

*Tafsiri: Yeyote ambaye amesoma kwa ikhlasi Salam chache atabaki bila kudhurika Siku ya Hukumu. Mamilioni ya Salamu ziwe juu ya Bwana wangu Kipenzi* صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم *kutoka kwangu! Ewe Muumba wangu* (عَزَّوَجَلَّ) *Mtumie Rasuli Wako Kipenz* صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم *ambaye ameniondolea matatizo na dhiki.*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mwenyezi Mungu sio mtegemezi (hategemei chochote)

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ni Muweza wa yote. Yeye عَزَّوَجَلَّ hategemei mtu yeyote. Yeye عَزَّوَجَلَّ ameuumba ulimwengu huu, akaupamba kwa vitu mbalimbali, na ameufanya ni mahala pa kuishi wanadamu humo, akidhihirisha Uwezo

Wake. Yeye عَزَّوَجَلَّ aliendelea kutuma Rusuli Yake na Ambiya عَلَيۡهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام duniani mara kwa mara kwa ajili ya mwongozo wa wanadamu. Akitaka عَزَّوَجَلَّ anaweza kuwafanya watu waovu warekebishwe hata bila ya Ambiya عَلَيۡهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام lakini yeye azzawajal ametaka waja wake wafikishe da'awah ya wema,wavumilie dhiki katika njia yake kisha wapate thawabu kubwa na vyeo vikubwa kwenye baraza lake. Kwa hivyo, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ aliendelea kutuma Rasuli wake na Ambiya عَلَيۡهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام katika ulimwengu kwa ajili ya kutekeleza kazi tukufu ya 'Da'awah ya wema' na hatimaye akamtuma kipenzi chake Nabii Muhammad صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم , kuhitimisha Nubuwwah. Kisha Yeye عَزَّوَجَلَّ akauachia kazi hii kubwa na tukufu kwa Ummah wa kipenzi, Mtume Wake Mtukufu صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم ili warekebishe wajibu huu muhimu kila mmoja wao kwa wao.

Hivyo kila Muislamu ni mhubiri; awe ni mwanachuoni au Imamu wa Msikiti, kiongozi wa kiroho au mwanafunzi, mfanyabiashara au mteja, mwajiri au mfanyakazi, afisa au kibarua, mtawala au mtu wa kawaida, bila kujali taaluma yake na hadhi ya kijamii, aendelee kukuza Sunnah, kufikisha 'mwito wa wema' kwa watu anaoishi au anaofanya nao kazi. Anapaswa kujitahidi kufanya kazi hii kubwa akitumia vyema uwezo wake.

*Mayn Muballigh banu Sunnataun ka*
*Khoob chercha karoon Sunnataun ka*

*Ya Khuda Dars doon Sunnataun ka*
*Ho karam bahr-e-khak-e-Madinah*

*Tafsiri: Naomba kuhubiri na kukuza Sunnah. Ewe Mwenyezi Mungu! Nibariki kwa uwezo wa kutoa Dars za Sunnah kwa wasila ya ardhi ya Madinah.*

صَلُّوۡا عَلَى الۡحَبِيۡب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Amri ya Qur'an ya 'Da'awah kwa wema'

Mwenyezi Mungu Mtukufu عَزَّوَجَلَّ ameelezea ubora wa da'awah ya wema katika sehemu mbalimbali za Qur'ani Tukufu. Hii hapa Aya ya 104 ya Surah Aal-e-'Imran, sehemu ya 4, pamoja na tafsiri yake kutoka ukurasa wa 128 wa Kanz-ul-Iman tukufu pamoja na Khaza`in-ul-'Irfan iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji wa Dawat-e-Islami.

Amesema Allah عَزَّوَجَلَّ:

وَلْتَكُنْ مِّنْكُمْ اُمَّةٌ يَّدْعُوْنَ اِلَى الْخَيْرِ وَيَاْمُرُوْنَ بِالْمَعْرُوْفِ وَيَنْهَوْنَ عَنِ الْمُنْكَرِ ؕ وَاُولٰٓئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُوْنَ ﴿۱۰۴﴾

*'Na liwe kundi miongoni mwenu linalolingania kwenye kheri, na linaloamrisha mema na linalokataza maovu hao ndio wenye kufaulu.'*

*[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 4, Surah Aal-e-'Imran, Ayah 104)*

## Kila mtu anapaswa kufikisha mwito wa haki kulingana na uwezo wake

Akitoa maoni yake juu ya Ayah iliyotajwa hapo juu, mfasiri mashuhuri wa Quran, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema katika kitabu Tafseer-e-Na'eemi, juzuu ya nne ukurasa wa sabini na mbili, Enyi waislamu! Pawepo na vuguvugu moja kama hilo miongoni mwenu, au muanzishe vuguvugu moja kama hilo kwa msingi wa kudumu ambalo linawalingania watu wote waovu kuelekea kwenye wema, makafiri kwenye imani ya Kiislamu, waasi kuelekea kwenye uchamungu, wenye kughafilika kuelekea kwenya utambuzi, wajinga kuelekea kwenye elimu ya Uislamu na Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ, waliohifadhiwa kuelekea kwenye radhi ya ibada (ya Mwenyezi Mungu) na walio katika usahaulifu kuelekea fahamu.

Vile vile, harakati hii inapaswa kutekeleza imani sahihi, tabia njema na matendo mema kwa kuhubiri, kwa maandishi, kimwili, madhubuti, laini na (mtawala kwa raia wake) kwa nguvu. Zaidi ya hayo, harakati hii inapaswa kuwazuia watu kutokana na imani potofu, tabia mbaya, matendo mabaya, nia mbaya na mawazo mabaya kwa ulimi na moyo, kwa maandishi na hata kwa nguvu (kulingana na mamlaka ya mtu).

## Kila mtu ni mhubiri !

Amesema zaidi yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه: Waislamu wote ni wahubiri. Ni Fard (wajibu) kwa wote kuwaamrisha watu kutenda mema na kuwaepusha na maovu (popote pale ambapo Shari'ah imetangaza kuwa ni Wajib kwao). *(Tafseer-e-Na'eemi, juzuu ya 4, uk. 72; imerekebishwa)*

Katika maelezo yake Mufti mtukufu رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه pia amenukuu Hadith zifuatazo kutoka katika kitabu Sahih Bukhari. Rasuli wa Rahmah, Muombezi wa Ummah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

amesema: ﴿بَلِّغُوْا عَنِّيْ وَلَوْ اٰيَةً﴾ *'Fikisheni kwa niaba yangu hata kama ni Aya moja.'* *(Sahih Bukhari, juzuu ya 2, uk. 462, Hadiyth 3461)*

*Mayn nayki ki da'wat ki dhoomayn macha doon*

*Ho taufeeq aysi 'ata Ya Ilahi*

*Tafsiri: Naomba kukuza na kueneza wito wa wema. Na nibarikiwe na uwezo huu ewe Mwenyezi Mungu!*

## Kitendo kinachowanufaisha wengine ni bora zaidi

Mfasiri mashuhuri, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema zaidi: Mahubiri(mawaidha) ya Kiislamu ni ibada muhimu sana. Matendo mengine yote ya ibada kwa kawaida humnufaisha mwabudu lakini mahubiri ya Kiislamu haimnufaishi mhubiri tu bali hunufaisha pia wengine. Kitendo kinachowanufaisha wengine badala ya mtendaji wake tu, ni bora kuliko kinachomnufaisha mtendaji wake tu. (Imepokewa katika riwaya kwamba) mtu alimuuliza Mtume صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم, 'Ni nani mja bora?' Yeye صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akajibu, '(Mja bora ni) yule ambaye anamkhofu Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ, na akawatendea wema jamaa zake, na anafikisha mambo mema (kwa watu) na anawaepusha na maovu.' *(Az-Zuhd-ul-Kabeer lil-Bayhaqi, uk. 327, Hadiyth 877)*

Sayyiduna Hasan Basri (رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه) amesema, 'Mwenye kuwaamrisha watu kufanya mambo ya kheri na kuwaepusha na maovu ni Khalifa wa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na Mtume wake na kitabu chake (yaani Kurani Tukufu).' Imeelezwa katika Hadiyth kwamba Waislamu wakiacha mahubiri ya Kiislamu, wafalme katili watawatawala na maombi yao hayatajibiwa. *(Ruh-ul-Ma'ani, juzuu ya 4, uk. 326)*

Kiongozi wa waumini, Sayyiduna Abu Bakr Siddiq رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ amesema, 'Enyi watu! Waamrishe wengine wafanye mema na wazuie na maovu, mtakuwa mnaishi maisha ya amani." Kiongozi wa Waumini, Sayyiduna Ali-ul-Murtada كَرَّمَ اللّٰهُ وَجْهَهُ الْكَرِيْم amesema,'da'awah ya wema ndio Jihad bora. *(Tefsir-i Kebir, 3. Cilt, Sayfa 316)*

Kuhubiri Uislamu ni ibada bora. Na kuiacha - (licha ya kuwa Wajib kwa Shari'ah) - ni uhalifu mbaya sana. Mwenye kuiacha atafedheheka. *(Tafseer-e-Na'eemi, juzuu ya 4, uk. 72; imerekebishwa)*

Kiongozi wa Waumini, Sayyiduna 'Ali-ul-Murtada كَرَّمَ اللّٰهُ وَجْهَهُ الْكَرِيْم pia amesema: "Moyo usiouona wema kama uzuri na uovu kama ubaya, utapinduliwa, kama vitu vilivyo ndani ya mfuko, vikipinduliwa,huanguka na kutawanyika. *(Musannaf Ibn Abi Shaybah, juzuu ya 8, uk. 667, Raqm 124, 125)*

## Majuto kwa maisha ya dhambi

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Siku hizi, dhambi zinatendwa kila mahali.Wakati mwingine, hata wale wanaoonekana kuwa wachamungu na wenye kujinyima raha hupatikana kuhusika katika imani potofu, mazungumzo ya ovyo, kutazama haramu na tabia mbaya. Ole! Dhambi zimekuwa ni za kawaida na zimeenea kila mahali! Ni kweli kwamba watu wacha Mungu bado wanapatikana duniani lakini ni wachache sana. Katika hali hiyo ya kusikitisha, kuwepo kwa vuguvugu lenye msukumo wa Sunnah 'Dawat-e-Islami' si chini ya fadhila kubwa, اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ.

Njoo ujiunge na mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami kwa ajili ya ulinzi wa imani yako na urekebishaji wa matendo yako. Hapa kuna fumbo la Madani kwa ushawishi wako.Ndugu wa Kiislamu kutoka Keamari Bab-ul-Madinah (Karachi) amesema: Nilikuwa nikiwatusi na kuwagombanisha watu katika mambo madogo.Nilipenda sana kutazama filamu na tamthilia na kusikiliza nyimbo na muziki.Nilikuwa nimepoteza sehemu kubwa ya maisha yangu katika dhambi hizi.Nilikuwa nikifanya kazi kama dereva wa mmiliki wa nyumba ya bungalow. Kilichonipelekea kutubu dhambi zangu ni kwamba siku moja baada ya kumaliza kazi yangu nilikaa chumbani ambapo nilisikiliza hotuba yenye msukumo wa Sunnah iliyokuwa ikionyeshwa kwenye Idhaa ya Madani. Hotuba hiyo ilinifanya nitetemeke kwa woga,na kunifanya nione aibu juu ya madhambi. Hakika nilitubia dhambi zangu kwa Mwenyezi Mungu, عَزَّوَجَلَّ na nilikusudia kwa dhati kutembelea njia ya Sunnah. Wakati tangazo la Tarbiyyati I'tikaf ya siku 30 katika mwezi mtukufu wa Ramadhani kwa ushawishi kwa Waislamu kuhudhuria, lilipotolewa kwenye Idhaa ya Madani, mara moja niliweka nia ya kuhudhuria I'tikafu, nikiitikia vyema.Kwa kutekeleza nia yangu, sasa ninavuna baraka za I'tikaf katika Madani Markaz ya kimataifa ya Dawat-e-Islami, Faizan-e-Madinah, Bab-ul-Madinah (Karachi).Pia nitasafiri na Madani Qafilah ya miezi 12 mara tu baada ya I'tikafu, اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Tiba ya dhambi

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Je, mmeona! Kwa baraka za kutazama Idhaa ya Madani, sio tu kwamba mtenda dhambi alipata tiba ya ugonjwa wa dhambi zake, bali pia aliweza kupata fursa ya kuhudhuria I'tikafu ya Tarbiyyati ya siku 30 katika mwezi mtukufu wa Ramadhani duniani. Madani Markaz wa Dawat-e-Islami, Faizan-e-Madinah, Bab-ul-Madinah (Karachi). Alibahatika zaidi kufanya nia ya kusafiri na Madani Qafilah yenye msukumo wa sunnah kwa ajili ya miezi 12 baada ya I'tikafu.

Kila mtu atafute tiba ya ugonjwa wa madhambi. Niamini! Tukifa bila ya kutubia licha ya kufanya madhambi mara kwa mara, na ikiwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ataukasirikia, hatutapata pa kujikinga kutokana na ghadhabu yake. Tabia za waja wema wa Mwenyezi Mungu ni za kipekee. Licha ya kutenda mema, wanamcha Mwenyezi Mungu, عَزَّوَجَلَّ na wanatafuta tiba ya madhambi. Sayyiduna Hasan Basri رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema kuwa siku moja alikuwa akifuatana na kijana mchamungu mahali fulani huko Basra alipomuona tabibu. Mbele ya tabibu huyo kulikuwa na umati mkubwa wa watu wakiwemo wanawake na watoto wakiwa na chupa za maji mikononi, wakisubiri kupata dawa za magonjwa yao. Yule kijana mcha Mungu akamuuliza mganga, 'Je, una dawa fulani ya madhambi?' Yule tabibu akajibu kwa kukubali. Yule kijana akasema, 'Tafadhali niambie tiba.' Tabibu akajibu: Tiba ya ugonjwa wa dhambi inahusu mambo kumi ambayo ni haya:

1. Chukueni mzizi kutoka kwenye mti wa ufukara na unyenyekevu.
2. Ongeza mchanganyiko wa toba kwake.
4. Weka kwenye bakuli la mapenzi ya Mungu.
5. Iponde ipasavyo kwa mshinikizo wa kuridhika.
6. Weka kisha kwenye sufuria ya uchamungu na kujinyima moyo.
7. Ongeza maji ya unyenyekevu kwake.
8. Kisha chemsha juu ya moto wa upendo wa Kimungu.
9. Kisha uimimine kwenye bakuli la shukrani.
10. Ipoze na shabiki wa matumaini.

11. Kisha unywe kwa kijiko cha sifa (ya Kimungu).

Ukifanya yote haya, basi kumbuka kwamba mapishi haya yatakufaa wewe kutibu kila maradhi na matatizo ya dunia na Akhera. *(Al-Munabbihat, uk. 111)*

*Kab gunahaun say kanara mayn karoon ga Ya Rab!*
*Nayk kab ay mayray Allah! Banu ga Ya Rab!*

*Kab gunahaun kay maraz wanasema mayn shifa paoon ga*
*Kab mayn beemar, Madinay ka banu ga Ya Rab!*

*Tafsiri: Lini nitaacha madhambi, Ewe Mola عَزَّوَجَلَّ! Lini nitakuwa mchamungu, Ewe Mola عَزَّوَجَلَّ! Ni lini nitapona ugonjwa wa dhambi! Ni lini nitakuwa mja wa Madina!*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Kula, kunywa na furahi

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Leo hii, kampeni mbaya za wasiokuwa Waislamu zinafanya juhudi za kunusurika na kueneza dini yao duniani lakini, ole wao Waislamu wamejiingiza katika mambo yao ya kidunia tu. Kwa kusikitisha sana, inaonekana kana kwamba Waislamu wengi wa leo wamefikiria kula tu, kunywa na kufanya sherehe kuwa lengo la maisha yao. Nani anajali kuwahubiria wengine kuhusu Swalah na Sunnah! Hawana hata wakati wa kusali Salah kwa utulivu kwa ajili ya kuboresha maisha yao ya baadae. Vipi wanaweza kuupata moyo uliojaa mapenzi kwa Sunnah! Leo, watu wengi wanajali maisha yao ya kidunia tu.

Imeelezwa katika ukurasa wa 103 wa kitabu chenye kurasa 125 'Shukr kay Fadaail' [i.e. Baraka za Shukurani], kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami: Sayyiduna Imamu Hasan Basri رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Mwenye kudhani kuwa chakula, vinywaji na nguo tu ndio neema za Mwenyezi Mungu , hakika ana elimu ndogo." *(Az-Zuhd li Ibn-ul-Mubarak, uk. 134, Raqm 397).*

*Dayta hoon Tujhay wasitah mayn piyaray Nabii ka*
*Ummat ko Khudaya rah-e-Sunnat pay chala day*

*Tafsiri: Ewe Mwenyezi! Ufanye Umma utembelee njia ya Sunnah kwa ajili ya Nabii Kipenzi na aliyebarikiwa* صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. *(Wasail-e-Bakhshish, uk. 100)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Sababu yenye kufurahisha ya kutopenda ulimwengu

Inasikitisha sana! Upendo kwa ulimwengu umeongezeka katika nyoyo zetu. Tunakimbilia kipofu anasa na starehe za ulimwengu. Kinyume chake, waja wema wa Mwenyezi Mungu na waja wa kweli wa Rasuli wangeshukuru [kwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ] kwa kukingwa na matamanio na neema za dunia. Sikiliza mfano wa mawaidha, uliochukuliwa kutoka ukurasa wa 68 wa kitabu 'Shukr kay Fadaail' na ujifunze somo: Sayyiduna Majma' Ansa رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesimulia kuwa kulikuwa na mchaMungu ambaye amesema, 'Fadhila ya kulindwa na starehe za dunia niliyopewa na Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ni kubwa kuliko maisha ya anasa ya kidunia kwa sababu Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ameichukia dunia kwa Rasuli wake Kipenzi صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Kwa hivyo, mimi nazithamini neema za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ambazo amezipenda kwa ajili ya kipenzi chake Mtume (Swalla Allaahu ‘alayhi wa aalihi wa sallam) صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم Kuliko zile ambazo hakuzipendelea kwa ajili ya mtume wake. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 4, uk. 117, Hadees 4489; muhtasari)*

Kuwa na mali na anasa za kidunia kwa wingi hakika ni fadhila lakini kuziepuka ni fadhila kubwa zaidi.

*Peechha mayra dunya ki mahabbat say chhura day*
*Ya Rab! Mujhay deewanah Muhammad ka bana day*

*Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu* عَزَّوَجَلَّ! *Niwezeshe niondoe mapenzi ya dunia na unifanye mja kwa Muhammad* صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Uislamu - kwa jina tu

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Hali inazidi kutoka kuwa mbaya hadi mbaya zaidi.

Inaonekana kana kwamba Uislamu umekuwepo kwa jina tu. Inasikitisha sana! Mtindo wa maisha wa Waislamu wengi ni kama wa wasio Waislamu. Sikiliza Hadiyth zifuatazo kwa makini sana ukitoa machozi kwa moyo wa huzuni, ikiwezekana. Sayyiduna Ali-ul-Murtada كَرَّمَ اللّٰهُ وَجْهَهُ الْكَرِيْم amesimulia kwamba Mtume wa Rahmah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Wakati utakuja juu ya watu ambao Uislamu utakuwa kwa jina tu na Quran kama Rasm (yaani. jadi) pekee. Masajid yao itakuwa imejaa [watu] lakini tupu ya Hidayah [mwongozo]; 'Ulamaa wao watakuwa watu waovu zaidi chini ya mbingu. Fitnah itatoka kwao na itarejea kwao. *(Shu'ab-ul-Iman, juzuu ya 2, uk. 311, Hadees 1908)*

## Waislamu - kwa jina tu

Akizungumzia juu ya Hadiyth iliotajwa hapo juu, mfasiri mashuhuri, mwanafikra mkubwa wa Ummah, Mufti Ahmad Yar Khan رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema (Uislamu utakuwepo kwa jina tu maana yake) kwamba majina ya Waislamu yatakuwa ya kiislamu na watajiita pia kama Waislamu, lakini mtindo wao wa maisha na sura zao zingekuwa kama zile za wasio Waislamu, kama inavyoonekana siku hizi. Inaweza pia kumaanisha kwamba majina na aina za dhahiri za nguzo za Uislamu zitakuwepo, lakini asili yao itakufa. Kwa mfano, Swalah itatekelezwa kwa dhahiri lakini hakutakuwa na unyenyekevu wa moyo na mwili. Zakah italipwa lakini hakutakuwa na ushirikiano na jamii. Hajj itafanywa lakini kwa ajili ya utalii. Jihad itafanyika lakini kwa ajili ya kupata madaraka na utawala.

Akitoa maoni yake kwa upande wa Hadiyth (Quran itakuwepo kama Rasm tu), Mufti mtukufu رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Neno la Kiarabu ﴿رَسْم﴾ [Rasm] limetumika vilevile katika Hadith iliyo hapo juu, ina maana bili, alama na jadi. Maana zote mbili hizi zinaweza kutumika hapa. Yaani alama za Quran zitachapishwa kwenye karatasi na maneno yake yatasemwa, lakini uchaji wake ndani ya nyoyo na kufuata maamrisho yake kutatoweka, au kwa njia nyingine, inaashiria kuwa Quran itatumika kwa kuapa kwa uwongo juu yake katika mahakama na kusomwa kwenye mazishi lakini sheria za Kikristo zitatekelezwa.

Sehemu ya Hadiyth (Masajid yao itajaa [watu] lakini tupu ya ibada) ina maana kwamba majengo ya Masajid yatajengwa kwa umaridadi sana kwa kuchongwa milango na kuta na vifaa vya kisasa vya umeme lakini hakutakuwa na mtu wa kuswali Swalah ndani yao. Maimamu wao watakuwa wapotofu. Kwa maneno mengine, Masajid itakuwa chanzo cha imani potofu badala ya mwongozo wa kweli. Sauti za wazungumzaji wapotovu

wanaotoa hotuba zitakuwa zikitoka kwa kila Msikiti kupitia vipaza sauti lakini hotuba hizo zitakuwa sumu kali ambayo itaeneza ukafiri na ukaidi [i.e. kutotii] kwa jina la mafundisho ya Quran.

Akizungumzia sehemu ya mwisho ya Hadiyth zilizobarikiwa, yeye رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه amesema, ‘Kutakuwa na idadi kubwa ya wanavyuoni wapotovu na wasio na vitendo ambao wataleta madhara makubwa, wakiwazunguka Waislamu wote kama kitu kimefungwa na kitu kingine. *(Mirat-ul-Manajih, juzuu ya 1, uk. 229)*

## Mwizi wa sanda husikia sauti kutoka kwa Ghayb

Kumbuka! Dars za Quran na Hadiyth na hotuba zenye msukumo wa Sunnah zilizotolewa na wanazuoni wa Kiislamu walioongoka huko Masajid hazijakosolewa katika ufafanuzi hapo juu. Kwa hakika Dars na hotuba za wanavyuoni hawa wa kweli wa Uislamu ni chemchemi ya uongofu unaoleta baraka na msamaha.

Sayyiduna Haatim Asam رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه siku moja alikuwa akitoa hotuba katika ‘Balkh’. Katika hotuba hiyo, رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه alifanya Du’a ifuatayo kwa ajili ya kuwatakia mema wakosefu, ‘Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Kwa fadhila Yako, msamehe mkosaji mkubwa wa Ijtima’ hii.’ Mwizi wa sanda pia alikuwepo katika Ijtima ile. Usiku, alienda makaburini kuiba sanda. Mara tu alipochimba kaburi, alisikia sauti ikitoka kwa Ghayb, ‘Ewe mwizi wa sanda! Umesamehewa leo katika Ijtima’ ya Haatim Asam; kwa nini unafanya dhambi hii tena usiku wa leo?’ Aliposikiliza hili, alilia na kutubu dhambi zake kwa unyoofu. *(Tazkira-tul-Awliya, uk. 222; muhtasari)*

*Mujhay day day Iman per istiqamat*
*Pa`ay Sayyid-e-Muhtasham Ya Ilahi*
*Mayray sar pay ‘isyan ka baar ah Maula!*
*Berha jata hay dam-ba-dam Ya Ilahi*
*Zameen baujh say mayray phatti nahin hay*
*Yeh Tayra hi toh hay karam Ya Ilahi*

*Tafsiri: Ewe Mwenyezi! Nibariki kwa uthabiti katika Imani kwa ajili ya Rasuli Mkuu* صَلَّى اللّٰهُ عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم*. Ole, mzigo wa dhambi unaongezeka mabegani mwangu kila dakika. Ewe*

*Mwenyezi! Ni kwa neema yako tu kwamba ardhi haipasuki kwa sababu ya mzigo wa dhambi zangu.* *(Wasail-e-Bakhshish, ukurasa wa 82)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Je, wasio Waislamu wanatuiga

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Ni fahari kubwa kwa maisha ya kidunia na vilevile ya baada ya kifo kuwaona wachamungu, kukaa pamoja nao, kusikiliza hotuba zao na kushiriki katika Ijtima'aat ya waja wa Rasuul. Mfano huu pia umetupa somo kwamba mhubiri anapaswa kuwahurumia wenye dhambi. Licha ya kuwausia, anapaswa pia kuwafanyia Du'a. Mfano huu ni wa zama za dhahabu za Tab'-e-Tabi'een.

Cha kusikitisha ni kwamba Waislamu siku hizi wamekuwa mbali na mafundisho ya Kiislamu. Cha kusikitisha ni kwamba Waislamu wengi leo wanajivunia kuwaiga wasiokuwa Waislamu, na kuacha Sunna. Pengine wamechukulia kuwa ni fadhila kuvaa mavazi yasiyo ya Kiislamu. Je, umewahi kuona mtu yeyote asiye Mwislamu mwenye mitindo halisi ya Kiislamu (kama ndevu zenye urefu wa ngumi, kilemba, mtindo wa nywele na mavazi yanayofuata Sunnah n.k.)? Kwa kweli haujaona. Hawa ni watu wajanja sana na wasio waaminifu ambao hawataacha njia zao za uwongo na chafu na hawatafuata Waislamu, lakini kwa masikitiko makubwa, ni Waislamu ambao wanaiga wasio Waislamu kwa ujinga. Enyi ndugu zangu wa Kiislamu mlioghafilika! Tafadhali rudini kwenye akili zenu! Kabla ya kukutana na kifo chako, amkeni kutoka katika usingizi wa kutojali na muwaamshe wengine pia! Kumbukeni!

*Na samjho gey to mit jao gey ay Musalmano!*
*Tumhari dastan tak bhi na hogi dastano mayn*

*Tafsiri: Enyi Waislamu! Ikiwa hautambui uzito wa hali hiyo, utafutiliwa mbali kutoka kwa uso wa dunia. Hata hadithi zako zitatoweka kwenye kumbukumbu za historia.*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mpenzi ambaye hakufanikiwa

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Hali ya Waislamu siku hizi haitajwi. Gharika ya dhambi inafagilia mbali kila mtu. Chini ya hali hizi muhimu, mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami, vuguvugu la kimataifa na lisilo la kisiasa la kuhubiri Quran na Sunnah, ni neema kubwa. Baki kuhusishwa nayo.

اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ Mabadiliko ya kushangaza na hata mapinduzi ya Madani hufanyika katika maisha ya wanaohusishwa nayo. Huu hapa ni mfano wa Madani unaoonyesha jinsi mapinduzi ya Madani yalivyofanyika katika maisha ya ndugu wa Kiislamu anayeishi katika eneo la Malir huko Bab-ul-Madinah (Karachi). Amesema: 'Kwa bahati mbaya, nilikuwa nimempenda msichana, ambaye alikuwa amenitupa kwenye pango la giza la dhambi. Siku moja, nilisikia kwamba alikuwa ameolewa na mtu mwingine. Habari hii ilifanya maisha yangu kuwa Jehanamu. Hatimaye, kama maelfu ya wapenzi wengine ambao hawakufanikiwa katika mapenzi yao,na kuangukia kucheza kwenye mikono ya Shetani, pia nikawa mraibu wa dawa za kulevya, pombe, kasumba na heroini. Hakungekuwa na kileo chochote ambacho sikuwa nimekunywa, nikidhani kimakosa kuwa hii ndio njia ya kutafuta faraja.

Nikiwa nimekatishwa tamaa na kuhuzunika sana, nilijaribu kujiua mara nyingi. Ili kujiua, nilikunywa kemikali, petroli na hata asidi lakini wakati wangu wa kufa ulikuwa haujafika. Ukarimu ulioje wa Mwenyezi Mungu! Licha ya dhambi zangu zisizohesabika, Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ hakunifungia mlango wa rehema. Jinsi nilivyobarikiwa ni kwamba niliwahi kukutana na mshiriki wa Rasool aliyehusishwa na mazingira ya Madani yenye harufu nzuri ya Dawat-e-Islami. Adabu na ukarimu wake zilinipa shauku kubwa kwa [i.e. maslahi katika] maisha. Mnamo tarehe 29 Sha'ban-ul-Mu'azzam 1427 AH (2006), kwa baraka za juhudi zake binafsi, nilipata fursa ya kuhudhuria Faizan-e-Madinah, Madani Markaz ya kimataifa ya Dawat-e-Islami. Nilishangaa kuona hali ya kiroho hapa. Kuona ndugu wa Kiislamu wakiwa wamevaa vilemba vya kijani, nilifurahishwa sana na imani yangu iliburudishwa.

Nilihudhuria I'tikaf ya siku 30 iliyofanyika katika mwezi wa Ramadhan-ul-Mubarak mwaka wa 1427 Hijiria. اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ Mimi, mtu mwenye dhambi, nilibarikiwa kwa kuchunga Siyam ﴿صِيَام﴾ katika Ramadhan-ul-Mubarak. Kwa baraka za mazingira ya Madani, niliondokana na tamaa ya mapenzi na mawazo machafu. Niliupamba uso

wangu kwa ndevu, kichwa kwa kilemba na mwili kwa mavazi ya kufuata Sunnah. Pia nikawa wa kawaida katika kutekeleza Swalah tano za kila siku. Wakati wa kuandika fumbo hili, ninashiriki katika shughuli za Madani kujaribu kujirekebisha nafsi yangu na watu wa dunia nzima.

*'Ataye Habib-e-Khuda Madani mahaul*
*Hay fayzan-e-Ghaus-o-Raza Madani mahaul*
*Ba-fayzan-e-Ahmad Raza* اِنْ شَآءَاللّٰه
*Yeh phoolay phalay ga sada Madani mahaul*

*Tafsiri: Mazingira ya Madani ni majaliwa ya Mungu. Ni neema ya Ghaus na Raza* رَحْمَةُاللهِ عَلَيْه *na itastawi daima,* اِنْ شَآءَاللّٰه عَزَّوَجَلَّ.

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Uharibifu wa upendo usio halali

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Je, uliona jinsi mpenzi anayeungua kwenye moto wa mapenzi ya kimahaba alivyotiwa msukumo wa kujiunga na mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami, na akabarikiwa kujitolea kwa Rasuli kama matokeo ya juhudi binafsi za mja wa Rasuli. Ni kwa fadhila za Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ kwamba aliiondoa; la sivyo, mtu anayejiingiza humo mara chache hupata njia ya kuepuka. Siku hizi, kuna mwelekeo unaokua kwa kasi wa mahaba ya kimapenzi. Sababu kuu yake ni kwamba Waislamu wengi hawana elimu ya lazima ya Kiislamu na wako mbali na mazingira ya kidini. Hii pia imesababisha mafuriko ya dhambi kila mahali. Kutazama hadithi za mapenzi na tamthilia kwenye TV, VCR na intaneti n.k., kusoma riwaya, majarida ya kila mwezi, muhtasari, hadithi za mapenzi na habari zinazohusiana na mapenzi kupita kiasi zinazochapishwa kwenye magazeti, kuhudhuria masomo ya pamoja katika shule na vyuo vikuu na kukutana kwa uhuru na kuzungumza na jamaa wasio Mahram ndio sababu za mapenzi miongoni mwa vijana wa siku hizi.

Mwanzoni, mapenzi ni ya upande mmoja lakini mwenzi mwingine anapojulishwa juu yake pia wakati mwingine huanguka katika mapenzi, na kusababisha dhoruba kali ya dhambi. Wapenzi hawa basi hujiingiza katika mazungumzo ya bila aibu kwenye simu na

hata kukutana peke yao, kubadilishana barua za mapenzi na zawadi, na kuahidiana kwa siri kuoana. Ikiwa wanafamilia wao watasababisha kizuizi chochote, wakati mwingine wanatoroka [i.e. wakimbie], na habari za kutoroka kwao zinachapishwa kwenye magazeti, na kuzitia fedheha familia zao. Wakati fulani, wanaoa kwa mahakama, lakini wakati mwingine wanavuka mipaka yote ya maadili hata bila ndoa, na kisha maiti za watoto haramu [i.e. watoto wasio halali] wa wapenzi hao wakatili ambao hawajafunga ndoa hupatikana wamelala kwenye takataka. Zaidi ya hayo, ikiwa hawawezi kukimbia, basi wanajiua. Aina hizi za habari mara nyingi huchapishwa kwenye magazeti.

## Sayyiduna Yusuf عَلَيْهِ السَّلَام ameepukana na mapenzi ya haramu.

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Siku hizi, watu wamekuwa mbali na elimu ya Kiislamu, wakitumbukia kwenye shimo zito la ujinga. Ili kuficha penzi lao chafu la kimahaba, baadhi ya wapenzi wanadiriki hata kusema kwamba Sayyiduna Yusuf عَلٰى نَبِيِّنَا وَ عَلَيْهِ الصَّلٰوة وَالسَّلَام pia alikuwa akimpenda Zulaykha. (Allah عَزَّوَجَلَّ atuepushe!) Hili ni kosa kabisa, na watu wasio na hekima wenye mitazamo kama hiyo wamekosea kabisa. Kutoa visingizio kuhusu maovu ya Nafs kwa kusema bila busara jambo lisilofaa kuhusu Nabii kwa ushawishi wa Shetani kunaweza kuwa hatari sana kwa imani ya mtu.

Kumbuka! Sayyiduna Yusuf عَلٰى نَبِيِّنَا وَعَلَيْهِ الصَّلٰوة وَالسَّلَام ni Nabii wa Mwenyezi Mungu, عَزَّوَجَلَّ na kila Nabii عَلَيْهِ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام ni Ma'soom [yaani amekingwa na kila aina ya dhambi na matendo ya aibu]. Nabii عَلَيْهِ الصَّلٰوة وَالسَّلَام kamwe hawezi kufanya jambo lolote lisilofaa. Hapa kuna Aya ya 24 ya Surah Yusuf pamoja na tafsiri yake kutoka ukurasa wa 445 wa Kanz-ul-Iman tukufu pamoja na Khaza`in-ul-'Irfan iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika sehemu ya 12 ya Qurani Tukufu:

وَلَقَدْ هَمَّتْ بِهٖ ۚ وَهَمَّ بِهَا لَوْلَاۤ اَنْ رَّاٰ بُرْهَانَ رَبِّهٖ ؕ

*Na kwa hakika yule mwanamke alielekea kwake; naye angeli mtamani lau kuwa hakuona dalili za Mola wake Mlezi.[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 12, Surah Yusuf, Ayah 24)*

Akizungumzia Ayah hiyo hapo juu, mfasiri mashuhuri wa Qur'an, 'Allamah Maulana Sayyid Muhammad Na'eemuddin Muradabadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Allah amewaepusha

Ambiya na tabia mbaya na vitendo viovu, na amewabariki kwa tabia na adabu njema. Hivyo wanajiepusha na kila uovu. Kwa mujibu wa riwaya, Zulaykha alipojaribu kumlawiti, Sayyiduna Yusuf عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام, alimuona baba yake Sayyiduna Ya'qoob عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام. aliyekuwa amekikandamiza kidole chake kati ya meno yake, na akawa anamuashiria Sayyiduna Yusuf عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام kukaa mbali naye.' *(Khaza`in-ul-'Irfan)*

Hakika ni kwamba yalikuwa mapenzi ya upande mmoja kutoka kwa Zulaykha tu, na Sayyiduna Yusuf عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام hakuwa amejishughulisha nayo hata kwa daraja la chini. Katika Aya ya 30 ya Surah Yusuf, sehemu ya 12, maneno ya baadhi ya wanawake wa Misri yamenukuliwa kama hivi:

وَ قَالَ نِسْوَةٌ فِی الْمَدِیْنَةِ امْرَاَتُ الْعَزِیْزِ تُرَاوِدُ
فَتٰىهَا عَنْ نَّفْسِهٖ ۚ قَدْ شَغَفَهَا حُبًّا ؕ اِنَّا لَنَرٰىهَا فِیْ ضَلٰلٍ مُّبِیْنٍ ﴿۳۰﴾

*Na baadhi ya wanawake wa mjini wakasema, 'Mke wa mtawala anataka kumshawishi kijana wake; hakika upendo wake umezidi ndani ya moyo wake; na tunamkuta amevutiwa na upendo usio na mipaka'.*

*[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 12, Surah Yusuf, Ayah 30)*

Hujjat-ul-Islam, Sayyiduna Imamu Abu Haamid Muhammad Bin Muhammad bin Muhammad Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Zulaykha alikuwa na shauku kwa Sayyiduna Yusuf عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام lakini yeye (Yusuf Alaihi salaam ) alimkwepa licha ya kuwa na uwezo. Katika Quran Tukufu, Allah عَزَّوَجَلَّ alimthamini sana kwa kumwepuka. *( Ihya-ul-'Uloom, juz. 3, uk. 129).*

## Wapenzi wasio na busara hukosea kabisa.

Hili limefahamisha kama mchana, ya kwamba udhuru uliotolewa kutokana na tukio la Sayyiduna Yusuf عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام na Zulaykha kwa wapenzi wasiyo na hekima katika mapenzi yao chafu na maovu ni dhidi ya Qur'ani Tukufu, na hupelekea moja kwa moja kwenye ukafiri katika hali nyingi. Sura Yusuf inataja mapenzi ya upande mmoja tu kwa upande wa Zulaykha; haikutaja hata dalili ya Sayyiduna Yusuf عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام kuhusika katika mapenzi. Kwa hiyo, wale ambao wana dhana potofu kwamba Sayyiduna Yusuf عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْہِ الصَّلٰوۃُ وَالسَّلَام naye pia alihusika katika mapenzi, watubie kutokana na Imani

hiyo. Ambiya عَلَيۡهِمُ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام wa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ wana hadhi ya juu sana na wamekingwa na madhambi.

Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Tubariki kwa kujitolea Kwako na Rasuli Kipenzi chako صَلَّى الله عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Ondoa ulimwengu mioyoni mwetu. Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Wakomboe Waislamu walionaswa katika mapenzi ya dhambi na haramu na uwafanye kuwa waja wa kweli wa Rasuli Wako Mpenzi.

اٰمِيۡن بِجَاهِ النَّبِيِّ الۡاَمِيۡن صَلَّى الله عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

*Mahabbat ghayr ki dil s ynikalo Ya Rasoolallah*
*Mujhay apna hi deewanah bana lo Ya Rasoolallah*

*Tafsiri: Ewe Rasoolallah* صَلَّى الله عَلَيۡهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم! *Ondoa mapenzi kwa wengine kutoka kwa moyo wangu na unifanye kuwa mpenzi wako.*

(Kwa maelezo ya kuvutia kuhusu 'mapenzi ya haramu', soma kutoka ukurasa wa 318 hadi 356 wa kitabu 'Parday kay Baaray mayn Suwal Jawab' [Maswali na Majibu kuhusu Pazia la Kiislamu] kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-islami).

## Hotuba ya dhati ya Imam Awza'ee.

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Hebu tusikilize hotuba ya dhati ya Sayyiduna Imam Awza'ee رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه. Hii itatia msukumo wa uchamungu, itaondoa kutojali na kulainisha moyo. Imeelezwa katika ukurasa wa 32 na 33 wa kitabu cha 'Shukr kay Fadaail' chenye kurasa 125 kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami: Alipokuwa akitoa hotuba, Sayyiduna Imam Awza'ee رَحۡمَةُ اللّٰهِ عَلَيۡه. alisema mara moja: Enyi watu! Kwa neema za kidunia, jilindeni na moto wa Mwenyezi Mungu uunguzao moyo. Hakika unaishi katika nyumba kama hii (yaani ulimwengu wa dunia) ambapo hata kukaa kwa muda mrefu ni mfupi sana. Umetumwa hapa kwa muda maalum kama warithi wa wale waliogeukia marembo na mavuto ya ulimwengu. Walikata hata milima na mawe na walikuwa wakitanga-tanga katika miji. Walikuwa na nguvu na miili kama nguzo. Waliishi muda mrefu kuliko wewe na walikuwa warefu

kuliko wewe. Waliacha ishara kubwa duniani. Pamoja na hayo yote, walisahaulika upesi na ishara zao zikafutika. Nyumba zao zilibomolewa na hakuna wa kuzitaja sasa. Huwaoni wala huwasikii. Walikuwa wametegemea matumaini ya uwongo na walitumia siku na usiku katika kutojali. Kisha adhabu ya Mwenyezi Mungu ikawekwa juu yao usiku, wakiwaacha wamelala kifudifudi majumbani mwao asubuhi. Wale walionusurika hawakuweza kufanya lolote isipokuwa kuona, kwa mshangao, adhabu ya Mwenyezi Mungu, kupoteza neema na kubomolewa nyumba.

Hili ni fundisho kwa wale wanaoogopa adhabu kali na wana khofu ya Mwenyezi Mungu katika nyoyo zao. Sasa maisha yako pia ni mafupi sana. Ulimwengu haudumu. Katika zama hizi, uvumilivu, msamaha na uungwana vinaonekana kutoweka. Kilichobaki ni matope ya maovu, vitisho, dalili za mateso, dhoruba za dhambi, matetemeko ya ardhi mfululizo, huzuni, kukata tamaa na warithi waovu. Athari mbaya za maovu yao zimejitokeza katika nchi kavu na baharini. Haupaswi kufuata wale ambao walitumia maisha kutimiza matamanio yao na walidanganywa na matumaini ya muda mrefu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ kwamba Atujumuishe katika wale wanaoweka nadhiri zao, wanatambua makazi yao halisi na wako tayari kwa hayo. *(Tareekh Dimashq li Ibn 'Asakir, juzuu ya 35, uk. 208, Raqm 3907)*

*Maut tehri aanay waali aaye gi*
*Jan tehri jaanay waali jaye gi*

*Ruh rag rag sema nikali jaye gi*
*Tujh pay ik din khak daali jaye gi*

*Qabr mayn mayyit uterni hay zaroor*
*Jaysi kerni waysi bherni hay zaroor*

*Tafsiri: Hakika utakutana na adhabu yako inayokaribia. Nafsi yako itaondolewa kutoka kwa kila mshipa. Hakika utazikwa kwenye kaburi lako ambapo utakuwa unavuna ulichopanda duniani.*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب        صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Utangulizi mfupi wa Imam Awza'ee

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Hivi punde tumesikiliza hotuba ya dhati ya Sayyiduna

Imam 'Abdur Rahman Awza'ee رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه. Yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alikuwa mwanachuoni mahiri, Mufti mkubwa na Imam mashuhuri sana kutoka Syria. Yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alitoa maelfu sabini ya Fatawa na alikuwa miongoni mwa Tab'-e-Tabi'een. Yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alizaliwa mwaka wa 88 Hijiria na alifariki dunia katika mwezi wa Rabi'-un-Nuur mwaka 157 Hijiria. *(Hilyat-ul-Awliya, juzuu ya 1, uk. 198)*

## Baraka ka tika ndoto

Sayyiduna Imam Awza'ee رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Wakati fulani nilibarikiwa kumuona Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ katika ndoto yangu. Allah عَزَّوَجَلَّ akasema, 'Ewe 'Abdur Rahman! Ni wewe unaowalingania watu kwenye wema na kuwaepusha na maovu?' Nikasema kwa unyenyekevu, 'Ndiyo, Ewe Muumba wangu Mwingi wa Rehema! Ni kwa neema Yako tu kwamba ninaweza kufanya hivyo. Ewe Muumba wangu! Niweke imara katika Iman wakati wa kuondoka kwangu duniani.' Allah عَزَّوَجَلَّ akasema, 'Katika njia ya Sunnah pia.' *( Hilyat-ul-Awliya, juz. 6, uk. 153, Raqm 8131).*

## Matukio ya ajabu ya kifo

Sayyiduna Imam Awza'ee رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه aliishi Beirut. Mara moja yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه aliingia Hammaam huko Beirut. Mmiliki wa Hammaam aliifunga bila kujali na akaenda zake. Baada ya siku chache, alipokuja na kuifungua, akamkuta Sayyiduna Imam Awza'ee رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amefariki dunia na amelala akielekea Qiblah huku mkono wake wa kulia ukiwa chini ya shavu lake. *(Ibn 'Asakir, juzuu ya 35, uk. 222)*

Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ amrehemu na atusamehe bila ya hesabu kwa ajili yake!

اٰمِيْن بِجَاهِ النَّبِيِّ الْاَمِيْن صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

*Sarkar-e-Madinah ki Sunnat pay jo chaltay hayn*
*Allah kay woh banday zindah hayn mazaraun mayn*
*Tafsiri: Wale waja wa Mwenyezi Mungu wanaofuata Sunnah za kipenzi chake Mtumewamo* صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم *hai katika makaburi yao.*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mnywaji (pombe) akawa Muazzin

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Ili kutambua lengo la maisha, kulifanikisha, kukuza fikra ya kufanya maandalizi ya kifo, na kuwa na shauku ya kuboresha maisha yako ya baada ya kifo na maisha ya kidunia, daima endelea kushikamana na mazingira ya kusukuma Sunnah ya kimataifa na isiyo ya kisiasa, mazingira ya Madani ya Dawat-e-Islami. Dawat-e-Islami ndiyo inayomtia moyo hata mtu mwovu kurekebishwa. Kusafiri pamoja na Madani Qafilah yenye msukumo wa Sunnah pamoja na waja wa Rasuli humfikisha hata mtu mbaya zaidi katika jamii hadi kwenye kilele cha maadili. Huu hapa ni muhtasari wa fumbo la ajabu lililosimuliwa na ndugu wa Kiislamu kutoka Maharashtra, India. Amesema: Kabla sijajihusisha na Dawat-e-Islami, nilikuwa ni mwenye dhambi kubwa sana. Ningefanya kazi siku nzima lakini ningepoteza pesa nilizopata kwa bidii katika kunywa (pombe). Ningefurahia maovu mbalimbali, kuwaita watu majina mabaya, na hata kuwaudhi wazazi wangu na majirani. Pia nilikuwa mcheza kamari sana na sikutekeleza Swalah yoyote. Nilikuwa nikipoteza bila kujali nyakati za thamani za maisha yangu.

Kwa bahati nzuri, niliwahi kukutana na ndugu wa Kiislamu anayewajibika wa Dawat-e-Islami. Akifanya juhudi ya kibinafsi, alinialika nisafiri na Madani Qafilah yenye msukumo wa Sunnah. Maneno yake matamu na ya dhati yalinigusa moyo, nami nikakubali mwaliko wake. Nilisafiri na Madani Qafilah yenye msukumo wa Sunnah kwa ajili ya siku 3 pale pale. Nikiwa pamoja na waja wa Rasuul, nilisikiliza hotuba kutoka kwenye vijitabu vilivyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami. Kwa baraka za Madani Qafilah, mcheza kamari na mnywaji pombe mzito kama mimi ambaye hakuwahi kuswali Swalah yoyote sio tu kwamba alianza kuswali bali pia alianza kuita Sada-e-Madinah (yaani kuwaamsha Waislamu kwa ajili ya Swalah- ul- Fajr).

Pia nina bahati ya kuwaalika wengine kusafiri pamoja na Madani Qafilah. اَلْحَمْدُ لِلّٰه عَزَّوَجَلَّ! Kutokana na juhudi zangu za kibinafsi, ndugu 30 wa Kiislamu hadi sasa wamesafiri katika Madani Qafilah. Sasa mimi ni Muazzin katika Masjid na ninashughulika kufanya juhudi katika shughuli za Madani.

*Chhorayn may-naushiyan mat bakayn gaaliyan*

*Aayain taubah karayn, Qafilay mayn chalo*

*Ay sharabi tu aa, Mil kay saaray karayn, Qafilay mayn chalo*
*aa juwari tu aa*
*Chhutayn bad-'aadatayn, Qafilay mayn chalo*
*Hoga lutf-e-Khuda, aao bhai Du'a*

*(Wasail-e-Bakhshish, uk. 615)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Adhabu kwa ajili ya dhambi iliyoelezwa katika mfano hapo juu

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Umeona! Mnywaji na mcheza kamari, ambaye alikuwa akiwasumbua wazazi wake na majirani, akiwaita watu kwa majina mabaya na ambaye hakuwahi kuswali Swalah yoyote, alitiwa moyo na juhudi za kibinafsi za mhubiri wa Dawat-e-Islami kusafiri katika Madani Qafilah yenye msukumo wa Sunnah, ambapo alisikiliza hotuba kutoka kwa vijitabu vya Madani akiwa na waumini wa Rasool. Akiwa amevutiwa, alitubu dhambi zake, akaanza kueneza Sunnah, kufanya Sada-e-Madinah na kuita Azan Msikitini na hivyo kuwaalika wengine kuswali. Zaidi ya hayo, hakuanza tu kusafiri katika Madani Qafilah mwenyewe bali pia kuwashawishi wengine kufanya vivyo hivyo.

Enyi waja wa Rasuli! Kumbuka kwamba ni Fard kwa kila Mwislamu wa kiume na wa kike mwenye akili timamu kuswali. Mwenye kuswali anastahiki Pepo, ambapo mwenye kukosa hata Swalah moja kwa hiari yake anastahiki adhabu ya moto kwa maelfu ya miaka. Mnywaji pombe na mcheza kamari wamefedheheka duniani na Akhera na wanastahiki adhabu kali katika Jahannamu. Usiku wa kupaa (mi'iraj), Rasuli wa Rahma صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم aliwaona wale waliowaasi wazazi wao wananing'inia kwa matawi ya moto. Kuna haki nyingi za majirani. Mtume (Swalla Allaahu 'alayhi wa aalihi wa sallam) صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema, "Mtu ambaye jirani yake hajasalimika na madhara yake hataingia Peponi." *[Sahih Muslim, uk. 43, Hadith 73{46} Kumwita muislamu majina mabaya ni kitendo cha Haramu kinachopelekea Motoni]*

## Wape watumishi chakula na mavazi kama yako

Hapa chini ni kifungu kilichofanyiwa marekebisho kidogo kutoka ukurasa wa 156 hadi

160 wa kitabu chenye kurasa 246 'Muntakhab Hadeesayn' [Ahadees Yaliochaguliwa] kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami. Kifungu hiki, Kwa kweli ni kuhusu kutumia maneno yasiyofaa na kuona aibu juu yake. Isikilize na upate lulu za Madani zenye kuburudisha imani.

Imeelezwa katika kitabu Sahih Bukhari kwamba Sayyiduna Ma'roor رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ amesema: Nilikutana na Sayyiduna Abu Zar Ghifari رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ katika Rabazah (mahali palipo kwenye umbali fulani kutoka Madinah). Yeye رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ na mtumwa wake walikuwa wamevaa vazi la aina moja. Nikauliza kuhusu hilo, basi yeye رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ akajibu: Niliwahi kugombana na mtu, nikimsema vibaya mama yake. Rasuli Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akaniambia, 'Ewe Abu Zar! Umeongea maneno ya kuudhi kuhusu mama yake; wewe ni mtu wa namna hiyo ambaye bado una sifa [zama za kabla ya Uislamu] za ujinga. Wajakazi na watumwa wenu ni ndugu zenu (wa kidini). Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ amewafanya kuwa chini yako. Yule aliye na ndugu yake chini yake ampe kile anachokula yeye mwenyewe na mavazi anayovaa yeye mwenyewe. Usiwasumbue waja hawa kwa kazi zinazowafanya wawe na huzuni, na ikiwa utawasababishia shida yoyote kama hiyo (kuwafanya wafanye kazi ngumu), basi wasaidie katika kazi. *(Sahih Bukhari, juzuu ya 1, uk. 23, Hadithi 30)*

## Majuto makubwa na msamaha wa kipekee.

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Mtu ambaye Sayyiduna Abu Zar رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ alikuwa ametumia maneno yasiyofaa juu yake ni Sayyiduna Bilal Habshi رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ Aliyoyasema رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ yalikuwa yasiyofaa tu, wala si ya aibu. Yeye رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ alikuwa amesema tu, 'Ewe mtoto wa mama mweusi'. Pale Sayyiduna Bilal رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ alipomlalamikia Rasuli Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم. Yeye صَلَّی اللّٰہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم akamkemea na kumnasihi Sayyiduna Abu Zar Ghifari رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ. Jinsi Sayyiduna Abu Zar رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ aliiitikia ni hadithi yenye kuvunja moyo. Sikiliza na utetemeke kwa hofu ya Kimungu.

Baada ya Sayyiduna Abu Zar Ghifari رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ kukemewa na Rasuli Mtukufu صَلَّی اللّٰہُ عَلَیۡہِ وَاٰلِہٖ وَسَلَّم alijawa na aibu na mara moja akamwendea Sayyiduna Bilal Habshi رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ, akaweka shavu lake zuri juu ya ardhi, akasema kwa unyenyekevu sana na kwa machozi katika njia ya kusihi, 'Ewe Bilal! Isipokuwa ukikanyaga shavu langu, sitalinyanyua kutoka ardhini.' Kwa kuhisi msukumo mkubwa, Sayyiduna Bilal رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ bila kupenda akaweka mguu wake kwenye shavu la Sayyiduna Abu Zar رَضِیَ اللّٰہُ عَنۡہُ na kuiondoa mara moja tu baada ya

hapo naye رضی اللّٰہ عنہ pia akamsamehe Sayyiduna Abu Zar Ghifari رضی اللّٰہ عنہ. *(Irshad-us-Saari, juzuu ya 1, uk. 197)*

## Sayyiduna Abu Zar Ghifari رضی اللّٰہ عنہ alikuwa mchamungu

Akizungumzia mfano huo hapo juu, Sayyiduna 'Allamah Qastalani رحمۃ اللّٰہ علیہ amesema: Sayyiduna Abu Zar Ghifari رضی اللّٰہ عنہ alisema maneno yale kwa sababu yeye رضی اللّٰہ عنہ alikuwa hajui kuwa yalikuwa Haraam. Lau yeye رضی اللّٰہ عنہ angelijua hilo, رضی اللّٰہ عنہ kamwe asingefanya hivyo. Rasuli Mpenzi na Mwenye Baraka صلی اللہ علیہ والہ وسلم pia alimkemea kwa kusema tu 'wewe bado unayo sifa ya [zama za kabla ya Uislamu] za ujahiliya'. Kemeo hili pia linaonyesha vyeo vyake vya juu. Ni kana kwamba yeye رضی اللّٰہ عنہ alishauriwa kwamba mtu mkubwa kama wewe hafai kusema jambo baya kama hilo. *(Ibid)*

## Uthabiti wa Sayyiduna Abu Zar Ghifari رضی اللّٰہ عنہ

Sayyiduna Abu Zar Ghifari رضی اللّٰہ عنہ ni miongoni mwa masahaba waliosilimu katika zama za mwanzo. Baadhi ya wanavyuoni رحمہم اللّٰہ hata wamesema, Yeye رضی اللّٰہ عنہ alikuwa wa tano katika maswahaba wasiokuwa Hijazi عرض المزید ی عنھم kusilimu. Tukio la kina la jinsi alivyosilimu رضی اللّٰہ عنہ limetolewa katika kitabu Sahih Bukhari. Yeye رضی اللّٰہ عنہ alikuwa na shauku kubwa juu ya Uislamu kiasi kwamba alitangaza Uislamu wake bila woga kila siku. Makafiri waliokasirika walikuwa wanamkimbiza na yeye رضی اللّٰہ عنہ, akiwa ametapakaa damu, akipoteza fahamu. Mara tu رضی اللّٰہ عنہ alipopata fahamu,Yeye رضی اللّٰہ عنہ alikuwa akitangaza jambo lile lile. Hii iliendelea kwa siku kadhaa. *(Muntakhab Hadeesayn, uk. 157)*

Mwenyezi Mungu عزوجل amrehemu na atusamehe bila ya hesabu kwa ajili yake!

*Khudaya ba-haq-e-Bilal-o-Abu Zar*

*Mujhay Deen kwa istiqamat 'ata ker*

*Ilahi na kuch poochhna rauz-e-Mahshar*

*Mujhay bakhsh bahr-e-Bilal-o-Abu Zar*

*Ilahi Baraye Bilal-o-Abu Zar*

*Mujhay Khuld mayn day jawaar-e-Payamber*

*Tafsiri: Ewe Mwenyezi! Nijaalie niwe na uthabiti katika Uislamu, nisamehe bila ya hesabu Siku ya Qiyaamah na unijaalie ujirani wa Kipenzi Chako na Mbarikiwa Rasuul* صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم *kwa wasila ya Sayyiduna Bilal na Sayyiduna Abu Zarr.*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mnyama wa kutisha atatokea karibu na Siku ya Hukumu

Tafadhali jaribu kutambua umuhimu wa Da'awah ya wema. Karibu na Siku ya Hukumu, watu wataacha kuwalingania wengine kwenye wema, na hakutakuwa na matumaini ya kurekebishwa. Soma Ayah 82 ya Surah An-Naml pamoja na tafsiri yake kutoka ukurasa wa 712 wa Kanz-ul-Iman tukufu pamoja na Khaza`in-ul-'Irfan iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika sehemu ya 20 ya Quran Tukufu:

وَاِذَا وَقَعَ الْقَوْلُ عَلَيْهِمْ اَخْرَجْنَا لَهُمْ دَآبَّةً

مِّنَ الْاَرْضِ تُكَلِّمُهُمْ ۙ اَنَّ النَّاسَ كَانُوْا بِاٰيٰتِنَا لَا يُوْقِنُوْنَ ﴿۸۲﴾

*Na itakapo waangukia neno, tutawatolea mnyama katika ardhi, atasema nao, kwa sababu watu hawakuziamini Ishara zetu.* *[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 20, Surah An-Naml, Ayah 82)*

## Mnyama anayezungumza mwenye sura ya ajabu karibu na Siku ya Hukumu

Akizungumzia Ayah hiyo hapo juu, mfasiri mashuhuri wa Qur'an 'Allamah Maulana Sayyid Muhammad Na'eemuddin Muradabadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Yaani watapata adhabu ya kiungu, adhabu ya Mwenyezi Mungu itakuwa wajib juu yao na sababu yao yoyote haitakubaliwa. Watu hawatafikisha mwito wa kuelekea kwenye haki wala kuzuia maovu na hakutakuwa na matumaini ya kurekebishwa.

Atakuwa ni mnyama mwenye sura ya ajabu, ambaye atatoka kwenye mlima wa Safa (uliopo Makkah Mukarramah) na atatangatanga kwa kasi katika miji yote. Itakuwa

inazungumza vyema na kuweka alama kwenye paji la uso la kila mtu. Itachora mstari mkali kwenye vipaji vya nyuso za Waumini kwa fimbo tukufu ya Sayyiduna Musa عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْهِ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام na itaweka muhuri mweusi kwenye paji la uso wa mkafiri kwa pete ya Nabii Suleiman عَلٰی نَبِیِّنَا وَ عَلَیْهِ الصَّلٰوةُ وَالسَّلَام Ameendelea kusema yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَیْه Itakuwa ikisema kwa uwazi ﴿هٰذَا مُؤْمِنٌ وَّ هٰذَا كَافِرٌ﴾ huyu ni Mu`min, na huyu ni kafir} Yeye رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَیْه ameendelea kusema: *(Hawakuiamini Qurani)*

## Mwenye kulia ataingia Peponi

Rasuli wa Rahmah, Mwombezi wa Ummah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم mara moja alifikisha mwito wa wema kwa maswahaba zake رَضِیَ اللهُ عَنْهُم wakati wa kusoma Surah At-Takasur akilia kwa khofu ya Mwenyezi Mungu. Sayyiduna Jareer Ibn 'Abdullah رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ amesema kwamba Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema: 'Nitasoma Surah At-Takasur mbele yenu, Atakayelia miongoni mwenu ataingia Peponi.' Kwa hiyo, akaisoma صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم Baadhi yetu tulilia lakini wengine hawakulia. Wale ambao hawakuweza kulia wakasema, 'Ewe Rasualallah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم! Tulijaribu kulia lakini hatukuweza.' Mtume Mpenzi na Mwenyezi Mungu na mwenye Baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema, 'Ninaisoma tena mbele yenu. Mwenye kulia, basi pepo ni kwa ajili yake, na asiyeweza kulia angalau aonekane kama mwenye kulia. *(Nawadir-ul-Usool, juzuu ya 1, uk. 611, Hadees 862)*

## Mtoto mwenye kuvutia

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Hadiyth hapo juu ina maelezo ya dhati ya mwito wa kuelekea kwenye haki uliotolewa na Mtume wetu Mpenzi na Mwenye Baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa namna ya kipekee. Vile vile inaonesha kuwa Rasuli Mkubwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم anaweza kupeana chochote kutokana na mamlaka aliyopewa na Mwenyezi Mungu, ndiyo maana yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akasema, 'Mwenye kulia ataingia Peponi.' Pia inahusu Surah At-Takasur iliyo na Ayah nane zilizotajwa katika sehemu ya mwisho ya Quran Tukufu. Mwenye kuisoma anapata ujira wa kusoma Ayah elfu moja. Sura hii ina maelezo ya kutetemesha moyo, ya kaburi, Akhera na Moto. Laiti tungejifunza tafsiri yake kutoka kwa Kanz-ul-Iman kwa moyo na kulia kila tunapoisikia au kuisikiliza. Hebu tusikilize mfano unaohuzunisha moyo wa mtoto ambaye alimshangaza kila mtu kwa kuwasilisha kwa vitendo wito wa wema uliokuwa umejaa hofu ya Mwenyezi Mungu! Mtu mwadilifu siku moja alimwona mtoto analia amesimama nje ya Madrasah. Alipoulizwa sababu ya

kulia, mtoto huyo alijibu, ‘Leo mwalimu wetu ametufanya tuandike baadhi ya Ayah kwenye vibao kama somo letu, ndilo jambo ambalo limenifanya nilie.’ Alisema hivyo, alionyesha ubao uliokuwa umeandikwa Ayah zifuatazo juu yake.

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِيۡمِ

*Kuanzia kwa jina la Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehema, Mwenye kurehemu.*

اَلۡهٰكُمُ التَّكَاثُرُ ۙ﴿۱﴾ حَتّٰى زُرۡتُمُ الۡمَقَابِرَ ؕ﴿۲﴾ كَلَّا سَوۡفَ تَعۡلَمُوۡنَ ۙ﴿۳﴾ ثُمَّ كَلَّا سَوۡفَ تَعۡلَمُوۡنَ ؕ﴿۴﴾ كَلَّا لَوۡ تَعۡلَمُوۡنَ عِلۡمَ الۡيَقِيۡنِ ؕ﴿۵﴾

*Mapenzi ya kutafuta mali ya ziada yalikuweka mpuuzi. Mpaka ukafika makaburini. Ndiyo hakika, hivi karibuni utakuja kujua! Tena, ndiyo hakika, hivi karibuni utakuja kujua! Naam, lau mngelijua kwa ujuzi wa yakini, msingelipenda mali.* *[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 30, Surah At-Takasur, Ayah 1-5)*

Mtoto aliendelea kulia. Akiwa amevutiwa sana na mtoto, yule mtu mwadilifu akasema: Mwana! Somo kutoka katika Sura hii bado halijakamilika. Kuna Aayah nyingine ambazo labda mtapewa kesho kama somo. Baada ya kusema haya, alisoma Ayah zilizobaki za Surah At-Takasur ambazo ni kama ifuatavyo:

لَتَرَوُنَّ الۡجَحِيۡمَ ۙ﴿۶﴾ ثُمَّ لَتَرَوُنَّهَا عَيۡنَ الۡيَقِيۡنِ ۙ﴿۷﴾ ثُمَّ لَتُسۡـَٔلُنَّ يَوۡمَئِذٍ عَنِ النَّعِيۡمِ ﴿۸﴾

*Hakika mtaiona Jahannamu. Tena, hakika utaiona kwa maono ya hakika. Basi siku hiyo mtaulizwa juu ya neema.* *[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 30, Surah At-Takasur, Ayah 6-8)*

Akiwa na hofu kubwa kwa kusikiliza maelezo ya Jahannam, mtoto alianguka chini akitetemeka na kujikunyata na kufariki dunia. Mwalimu alikimbia na kumshika mtu mwadilifu. Watu walikusanyika, na wazazi wa mtoto aliyekufa pia walikuja. Akishtakiwa kwa mauaji, mtu huyo mwadilifu alishitakiwa mbele ya kadhi. Kadhi alimuuliza yule mtu mwadilifu kama alitaka kutoa maelezo yoyote katika utetezi wake. Mtu mwadilifu alisimulia hadithi yote. Kuisikiliza, Kadhi hatimaye akahukumu kwamba mtoto huyo alikuwa mchamungu sana na alikuwa ameuawa kishahidi kwa upanga wa hofu ya Mwenyezi Mungu. Kisha yule mtu mwadilifu aliachiliwa kwa heshima. *(Imefupishwa kutoka: Nuzhat-ul-Majalis, juzuu ya 2, uk. 94)*

Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ awarehemu na atusamehe bila ya hesabu kwa ajili yao!

اٰمِیْن بِجَاہِ النَّبِیِّ الْاَمِیْن صَلَّی اللهُ عَلَیْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم

*huda Madani munnay kay khauf-e-Khuda per fida*
*Suntay hi aayatayn dhayr jo ho gaya*

*Kash! Mil jaye mujh ko bhi aysi wila*
*Mayray mernay ka baa'is ho khauf-e-Khuda*

*Tafsiri: Jinsi hofu ya Mwenyezi Mungu ilivyokuwa ya kustaajabisha kwa mtoto aliyefariki kwa kusikiliza Ayah. Laiti ningepewa baraka kama hiyo kwamba ningefariki kutokana na hofu ya Mwenyezi Mungu.*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mtume Mtukufu ﷺ alifikisha wito kwa wema karibu na kaburi

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Sikiliza Hadiyth zinazopasua moyo zenye da'awah ya wema uliowasilishwa na Rasuli Mpenzi na Mwenye Baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akilia kwa khofu ya Mwenyezi Mungu. Imefafanuliwa katika kitabu Ibn Majah ni Hadiyth iliyopokelewa na Sayyiduna Bara Bin 'Aazib رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُ Akasema رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُ: Tulishiriki katika mazishi pamoja na Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم. Akiwa amekaa kando ya kaburi, صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم akalia sana mpaka ardhi ikalowa machozi yaliyokuwa yakitoka kwenye macho yake yenye baraka. Yeye صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kisha akasema, 'Fanyeni maandalizi kwa ajili yake. *(yaani kaburi).' (Sunan Ibn Majah, juzuu ya 4, uk. 466, Hadees 4195)*

## Sayyiduna 'Usman-e-Ghani alilia alipoona kaburi

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Licha ya kukingwa na kila aina ya adhabu ya kaburi na Siku ya Kiyama, Rasuli Mpenzi wangu na Mbarikiwa صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم alilia kwa khofu ya Mwenyezi Mungu wakati wa kulitaja suala la kaburi. Kadhalika, licha ya kuandikiwa kuingia Peponi, kiongozi wa waumini, Zun-Nurayn, mkusanyaji wa Quran Sayyiduna 'Usman Ibn 'Affaan رَضِیَ اللّٰہُ عَنْہُ hakuweza kujizuia [kuzuia] machozi wakati wa kutembelea makaburi.

Imeelezwa katika ukurasa wa 139 wa kitabu cha *'Allah Walon ki Baatayn'* chenye kurasa 695 (Juzuu ya 1) kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami: (Sayyiduna) Haani رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ. mtumwa wa Sayyiduna 'Usman-e-Ghani رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ, amesema kwamba Sayyiduna 'Usman-e-Ghani رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ, wakati wowote akisimama kando ya kaburi angelia sana hivi kwamba ndevu zake zilizobarikiwa zingelowa na machozi.' *(Sunan-ut-Tirmizi, juzuu ya 4, uk. 138, Hadees 2315)*

Katika kitabu Al-Mawa'iz-ul-'Asfooriyah ﴿اَلْمَوَاعِظُ الْعَصْفُوْرِيَه﴾, mfano huu umeelezwa kwa undani fulani. Kwa hiyo, alipoulizwa sababu ya kulia sana kuliona kaburi,yeye رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ akajibu, 'Nafikiri juu ya upweke wangu; hakuna atakayekaa nami katika kaburi langu.'*(Kisha, akifikisha da'awah ya wema)* رَضِیَ اللّٰهُ عَنْهُ akasema: Yule ambaye dunia ni kama jela yake, atalikuta kaburi lake ni Pepo, na yule ambaye kwake dunia ni kama Pepo ataipata kaburi lake kuwa jela. Kifo ni ujumbe wa kuachiliwa kwa yule ambaye maisha yake ya kidunia yalikuwa kama kifungo. Mwenye kujiepusha na matamanio ya Nafs duniani atapata malipo yake kamili huko Akhera. Mtu bora ni yule anayeondoka duniani kabla ya ulimwengu kumuacha, na ambaye ameridhika na Muumba wake (عَزَّوَجَلَّ) kabla ya kukutana Naye. Kila mtu atatendewa katika kaburi lake kama maisha yake ya kidunia. Yaani akitumia maisha yake kufanya mambo ya kheri atapata raha ndani ya kaburi lake lakini akikutana na kifo chake akifanya maovu atakumbana na adhabu. *(Maw'izah Hasanah, uk. 61-62)*

## Kaburi linaweza kuwa bustani au moto

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Waja wema wa Mwenyezi Mungu walikuwa wakiitafakari sana hali ya ndani ya kaburi. Kwa upande mwingine, ole, mara nyingi tunaona makaburi lakini hatujifunzi somo lolote. Laiti tungefikiria pia kwa uzito juu ya kaburi letu. Kumbuka! Makaburi yanayofanana kutoka kwa nje sio sawa kutoka ndani. Kaburi la mtu mmoja ni bustani nzuri wakati kaburi la mtu mwingine limejaa moto, nyoka na nge. Pia kumbuka kuwa uwezo wa kuhisi wa marehemu utabaki sawa kaburini. Kwa hiyo, waja wema wa Mwenyezi Mungu wanaoyaacha maisha haya katika hali ya Iman hukutana na rehema ya Mwenyezi Mungu, عَزَّوَجَلَّ wakifurahia starehe kubwa zisizo na kipimo kaburini. Lakini wale wanaomkasirisha Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na Rasuli wake صَلَّى اللّٰهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم kwa kuishi maisha ya dhambi wanakabiliwa na matatizo yasiyo mithilika wanapozikwa kaburini. Kwa kuwa uwezo wa kuhisi na akili ziko kaburini, marehemu anahisi na kuelewa kila kitu. Nguvu ya kuona na kusikia huongezeka kwa kiasi kikubwa,

na marehemu ana uwezo wa kutosha wa kuona na kusikia mambo tofauti. Anawaona wazi ndugu na marafiki zake wakirudi nyumbani wakiwa wamemzika. Anasikia hata nyayo zao.

## Upweke kaburini

Hebu fikiria! Hata kama haitolewi adhabu kwa mtenda dhambi; na anazikwa peke yake kwenye kaburi lenye giza, naapa kwa Mwenyezi Mungu, عَزَّوَجَلَّ hata hili linakuwa somo kubwa la kujifunza. Fikiria jinsi atapitisha wakati. Je, hali yake itakuwaje katika kaburi la kutisha, la kuhofisha na la giza? Kila mtu mwenye busara anaweza kutambua angalau kwa kiasi fulani. Hii ni kwa ajili ya kutufanya tutambue hali muhimu ya kaburi la sivyo mwenye dhambi anaweza kupata adhabu kali sana. Sayyiduna Masrooq رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Iwapo mwizi au mnywaji tembo au mzinifu [i.e. mwenye kufanya tendo la ndoa nje ya ndoa] akifa [bila ya kutubu], anapigwa na nyoka wawili wanaoendelea kuuma nyama yake na kuila." *(Kitab Zikr-ul-Maut ma' Mawsu'ah Imam Ibn Abid Dunya, juz. 5, uk. 476). Raqm 257)*

Hebu fikiria! Ikiwa mtu atafungwa akiwa hai gizani, kaburi la kutisha na la kuhofisha kama adhabu ya kukosa Swalah mara moja tu au kusema uwongo mara moja au kutazama haramu mara moja au kusikiliza wimbo mara moja au kutazama filamu mara moja au kumtaja mtu yeyote mara moja au kumkemea mtu kwa hasira. mara moja bila idhini ya Shari au kunyolewa ndevu mara moja, hali yake itakuwaje? Hakika watu wamchao Mwenyezi Mungu hutetemeka hata wakiifikiria. Ikiwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ amechukizwa, ni nani awezaye kubeba adhabu kaburini? Imeelezwa katika kitabu *(Hilyat-ul-Awliya)*, 'Mja anapozikwa kaburini, mambo hayo yote yanamjia kumtia khofu,aliyokuwa akiyaogopa duniani, lakini hakumuogopa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ. *(Hilyat-ul-Awliya, juzuu ya 10, uk. 12, Raqm 14318)*

Tunajikinga kwa Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ na adhabu ya kaburi na Moto.

*Ker lay taubah Rab ki rahmat hay bari*
*Qabr mayn wernah sasa hogi kari*
*Tubuni kwani rehema ya Mwenyezi Mungu ni kubwa*
*Ama sivyo adhabu kaburini itakuwa kali*
*(Wasail-e-Bakhshish, uk. 667)*

## Usidanganywe na ujana wako

Akifanya juhudi binafsi na kufikisha da'awah ya wema, Sayyiduna Mansur Bin 'Ammar رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه aliwahi kumuusia kijana mmoja kwa maneno haya: Ewe kijana! Haupaswi kudanganywa na ujana wako. Vijana wengi walijiingiza katika matumaini ya muda mrefu, wakasahau kifo chao na kuchelewesha na kupuuza toba, wakisema 'nitatubu kesho au kesho kutwa'. Hatimaye walizikwa kwenye makaburi yao na hawakunufaika na mali zao, watumwa, wazazi na watoto wao. Imeelezwa katika Aya ya 88 na 89 za Surah Ash-Shu'ara, sehemu ya 19:

يَوْمَ لَا يَنْفَعُ مَالٌ وَّلَا بَنُوْنَ ﴿۸۸﴾ اِلَّا مَنْ اَتَى اللّٰهَ بِقَلْبٍ سَلِيْمٍ ﴿۸۹﴾

*Siku ambayo hayatafaa mali wala wana. Isipokuwa yule aliye jihudhurisha mbele ya Mwenyezi Mungu na moyo ulio sawa.* *[Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 19, Surah Ash-Shu'ara, Ayah 88-89)*

*Milay khak mayn ahl-e-shan kaysay kaysay*
*Makeen ho gaye la-makaan kaysay kaysay*

*Huway naamwar bay-nishan kaysay kaysay*
*Zameen khha gayi nojawan kaysay kaysay*

*Jagah jee laganay ki dunya nahin hay*
*Yeh 'ibrat ki ja hay tamashah nahin hay*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب     صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## 'Qalb-e-Saleem' ni nini?

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! 'Qalb-e-Saleem', yaani moyo uliolindwa unamaanisha usafi wa moyo kutokana na imani potofu. Akizungumzia Ayah hiyo hapo juu, mfasiri mashuhuri wa Qur'an 'Allamah Maulana Sayyid Muhammad Na'eemuddin Muradabadi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Mwenye kujiepusha na ushirikina na ukafiri, atafaidika na mali yake aliyoitumia katika njia ya Mwenyezi Mungu na kizazi chake chema. Imeelezwa katika Hadiyth, 'Anapokufa mtu, amali zake hukatizwa isipokuwa mambo matatu – thawabu

yenye kuendelea, fedha zinazowanufaisha watu na watoto wachamungu wanaomfanyia Du'a. *(Sahih Muslim, uk. 886, Hadiyth 1631; Khaza`in-ul-'Irfan, uk. 593)*

*Meezan pay sab kharay hayn a'maal tul rahay hayn*
*Rakh lo bharam khudara 'Attar Qaadiri ka*

*Tafsiri: Wote wamesimama kando ya mizani na matendo yanapimwa. Okoa 'Attar Qaadiri kutokana na fedheha kwa ajili ya Mwenyezi Mungu* عَزَّوَجَلَّ.

*(Wasail-e-Bakhshish, uk. 195)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب      صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mapenzi ya mambo matano na kutojali mambo matano

Hizi hapa lulu tano za Madani zikifikisha da'awah ya wema na kutuamsha kutoka katika kughafilika. Amesema Rasuli wa Rahmah, Mwombezi wa Ummah, Mmiliki wa Jannah صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: ﴿سَيَأْتِيْ زَمَانٌ عَلٰى اُمَّتِيْ يُحِبُّوْنَ خَمْسًا وَّ يَنْسَوْنَ خَمْسًا﴾ Zama zitaujia Ummah wangu hivi karibuni watakapopenda mambo matano na watasahau mambo matano:

1. ﴿يُحِبُّوْنَ الدُّنْيَا وَ يَنْسَوْنَ الْاٰخِرَةَ﴾: Wataipenda dunia na wataisahau Akhera.

2. ﴿وَ يُحِبُّوْنَ الْمَالَ وَ يَنْسَوْنَ الْحِسَابَ﴾: Watapenda mali na watasahau uwajibikaji.

3. ﴿وَ يُحِبُّوْنَ الْخَلْقَ وَ يَنْسَوْنَ الْخَالِقَ﴾: Watawapenda viumbe na watamsahau Muumba.

4. ﴿وَ يُحِبُّوْنَ الذُّنُوْبَ وَ يَنْسَوْنَ التَّوْبَةَ﴾: Watapenda dhambi na watasahau toba.

5. ﴿وَ يُحِبُّوْنَ الْقُصُوْرَ وَ يَنْسَوْنَ الْمَقْبَرَةَ﴾: Watapenda majumba na watayasahau makaburi. *(Mukashafa-tul-Quloob, uk. 34)*

*Woh hay 'aysho 'ishrat ka koi mahal bhi*
*Jahan taak mayn hergharihoajal bhi*

*Bas ab apnay ni jahl kusema tu nikal bhi*
*Yeh jeenay ka andaz apna badal bhi*

*Jagah jee laganay ki dunya nahin hay*
*Yeh 'ibrat ki ja hay tamashah nahin hay*

*Tafsiri: Je, mtu anapaswa kufanya sherehe mahali ambapo yuko katika hatari ya kifo nyakati zote? Lazima sasa utoke kwenye giza la ujinga na ubadili mtindo wako wa maisha kwa sababu ulimwengu sio mahali pa kufurahiya bali kujifunza masomo.*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Toba ya nyimbo na muziki

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Ili kupata radhi ya Mwenyezi Mungu, kukuza hofu ya Mwenyezi Mungu moyoni, kuongeza shauku ya ulinzi wa imani, kutafakari juu ya kifo, kuhisi hofu kutokana na adhabu ya kaburi na Moto, kuondoa tabia ya dhambi, kufanya amali kwa uthabiti juu ya Sunnah, kuwasha mshumaa ya mapenzi kwa Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم moyoni na kuongeza shauku yako kwa ajili ya ujirani wa Mtukufu Mtume صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم katika Jannat-ul-Firdaus, daima endelea kuwa na uhusiano na Dawat-e-Islami, vuguvugu la kimataifa na lisilo la kisiasa la kuhubiri Quran na Sunnah. Safiri kila mwezi kwa angalau kwa siku tatu pamoja na Madani Qafilah wenye msukumo wa Sunnah pamoja na waja wa Rasuol, jaza kijitabu cha Madani In'amaat kila siku kinachofanya Fikr-e-Madinah na umkabidhi mtu husika tarehe ya kwanza ya kila mwezi wa Madani.

Huu hapa ni mukhtasari wa fumbo la Madani kwa ushawishi wako. Ndugu wa Kiislamu kutoka Hyderabad Bab-ul-Islam (Sindh) amesema: Nilikuwa kijana maridadi nikifurahia haiba na vivutio vya ulimwengu. Nikiwa nimezama katika matendo maovu na machafu kama vile nyimbo, muziki, filamu na tamthilia n.k., nilikuwa mbali na Swalah na Sunnah. Kwa bahati nzuri, Idhaa ya Madani ilizinduliwa mwezi wa *Ramadhani-ul-Mubarak 1429 AH (2008).* Kwa rehema za Allah عَزَّوَجَلَّ ,nilitazama vipindi vilivyorushwa kwenye Idhaa ya Madani. Nilivutiwa sana, nilianza kutazama mfululizo wake mwingi. Wakati fulani nilibahatika kutazama hotuba yenye msukumo wa Sunnah 'Nge Weusi'. Nikiwa nimeingiwa na woga wa Mwenyezi Mungu, mara moja nikaweka nia ya kufuga

ndevu usoni mwangu. Hotuba ya 'Nyimbo 35 za Kukufuru' ilipopeperushwa kwenye Idhaa ya Madani, nilitubu kutokana na nyimbo kwa woga papo hapo.

Wakati Bay'at ilifanywa kwenye Kituo cha Madani, اَلْحَمْدُ لِلّٰہ عَزَّوَجَلَّ nikawa mwanafunzi wa Mheshimiwa Ghaus-e-A'zam Sayyiduna Shaykh 'Abdul Qaadir Jeelani. Kwa fadhila za Allah عَزَّوَجَلَّ, nimeanza kuswali mara tano kila siku. Wakati wa kutoa kipande hiki cha maandishi, nimebarikiwa zaidi na bahati ya kufanya I'tikafu ya siku 30 iliyofanyika Ramadhani-ul-Mubarak chini ya usimamizi wa Dawat-e-Islami katika Faizan-e-Madinah ya kimataifa Markaz ya Dawat-e-Islami.

*Madani Channel Sunnataun ki laye ga ghar ghar bahaar*
*Madani channel say hamayn kyun walihanah ho na piyar*

*Ay gunahaun kay mareezon! Chahtay ho ger shifa*
*On kertay hi raho tum Madani Channel ko sada*

*Is mayn 'isyan say hifazat ka bahut saaman hay*
اِنْ شَآءَاللّٰہ *Khuld mayn bhi dakhilah aasan hay*

*Tafsiri: Tunaipenda sana Idhaa ya Madani kwa sababu inaleta chemchemi ya Sunnah kwa kila nyumba. Enyi wakosefu! Ukitaka kupona ugonjwa wa madhambi endelea kutazama Chaneli ya Madani. Itakukinga na madhambi na itakupeleka Peponi,* اِنْ شَآءَاللّٰہ عَزَّوَجَلَّ. *(Wasail-e-Bakhshish, ukurasa wa 605-606)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Kulia kwa khofu ya Mwenyezi Mungu wakati wa kufikisha da'awah ya wema

Wacha Mungu waliotangulia رَحِمَهُمُ اللّٰه wasingekosa fursa yoyote ya kuwalingania watu kwenye wema. Hata wakati wa kutembea au kusafiri, walikuwa wakifikisha da'awah ya wema. Sayyiduna Ibrahim Ibn Bashshaar رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Mimi na Fasawi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه tulikuwa tunaenda Shamu, akaja mtu ghafla na kusema baada ya kutusalimia, 'Ewe Abu Yusuf! Nipe nasaha.' Aliposikia haya, رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه akalia kisha akasema akifikisha da'awah ya wema, 'Ewe ndugu! Kuja na kwenda mara kwa mara kwa siku na usiku kunaonyesha

kuwa mwili wako unadhoofika, umri wako unaisha na kifo chako kinakaribia haraka. Ewe ndugu yangu! Ni lazima usiridhike isipokuwa kama umejua kwa hakika kwamba utakuwa na mwisho mwema. Kamwe msighafilike kwa sababu hamjui mtaingia Peponi au Motoni, na kama Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ yuko radhi nanyi kwa sababu ya rehema na fadhila zake au amekuchukieni kwa sababu ya dhambi zenu na kughafilika kwenu. Ewe mtu dhaifu! Usisahau kile ambacho wewe ni kwa hakika. Ulikuwa tone najisi hapo mwanzo na utakuwa maiti iliyooza mwishowe. Ikiwa huwezi kutambua kina cha ushauri wangu sasa, utatambua upesi ukizikwa kwenye kaburi lako ambapo utahisi aibu lakini haitakuwa na manufaa.'

Akisema hivyo رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه akanyamaza na kuanza kulia. Akiwa amezidiwa na hisia, mtu huyo aliyekuwa akitafuta ushauri pia alianza kulia. Msimulizi anaendelea kusema kwamba wote wawili walilia sana hadi wakapoteza fahamu. Kuona hivyo, msimulizi naye alilia. *(Zamm-ul-Hawa, uk. 437; muhtasari)*

*Mujhay sachchi taubah ki taufeeq day day*
*Pa`ay Tajdar-e-Haram Ya Ilahi*

*Jo naraz Tu ho gaya to kaheen ka*
*Rahun ga na Tayri qasam Ya Ilahi*

*Tafsiri: Ewe Mwenyezi! Nibariki mimi na toba ya kweli kwa ajili ya Kipenzi chako Mtume* صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم*. Ikiwa umenichukia, nitahukumiwa.* *(Wasail-e-Bakhshish, ukurasa wa 82)*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب　　صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Lia unapomwona mtu analia

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Je, umeona khofu ya Mwenyezi Mungu kwa watangulizi wetu wachamungu رَحِمَهُمُ اللّٰه? Wakati wa kufikisha Da'awah ya wema, wakati fulani walikuwa wakilia kwa khofu ya Mwenyezi Mungu. Ikiwa mtu yeyote hata leo atalia kwa khofu ya Mwenyezi Mungu wakati wa kufikisha da'awah ya wema au kutoa hotuba au kufanya Du'a au kusoma Qur'ani au Na'at, hakika hii ni fadhila kubwa kwake. Kujenga maoni hasi juu yake kumchukulia kuwa ni mtu wa kujikweza ni kitendo cha Haramu kinachoongoza kwenye Moto wa Jahannam. Kwa hivyo, hakuna mtu anayepaswa

kuunda maoni hasi. Wale wanaowaka moto wa hasira kwa sababu ya kuunda maoni mabaya juu ya wengine hawatapata chochote isipokuwa maangamizi yao wenyewe.

Sayyiduna Makhool Dimashqi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه alisema, 'Unapomwona mtu analia, nawe pia lia pamoja naye. Usijenge maoni hasi kwamba analia kwa kujionyesha. Mara moja nilipojenga maoni hasi kuhusu Mwislamu anayelia, hivyo sikuweza kulia kwa mwaka mmoja kama adhabu.' *( Tanbih-ul-Mughtarrin, uk. 107)*

*Yaad-e-Nabi mayn ronay wala ham deewano ko*
*Lakh paraya ho woh phir bhi apna lagta hay*

صَلُّوْا عَلَى الْحَبِيْب صَلَّى اللّٰهُ عَلٰى مُحَمَّد

## Mwenye kujionyesha ni mjinga mkubwa

Kudhania bila dalili sahihi kwamba mtu anayelia katika Du'a n.k. anajikweza [i.e.kujionyesha] bila shaka ni dhambi inayoelekeza Motoni, lakini mtu anayelia anapaswa kutafakari kwa uzito kwa nini analia. Ikiwa anashuku hata kidogo juu ya kujionyesha, anapaswa kuepuka kulia. Kwa hakika mtu mwenye kujikweza ni mjinga kwani anahatarisha thawabu kubwa alizopewa na Mwenyezi Mungu kwa ajili ya starehe ya muda ya kusifiwa, kusifiwa na kuchukuliwa na watu kuwa ni mchamungu. Jambo baya hata zaidi ni kwamba, mtu huyo mwenye majivuno mwenye kuchukiza mara nyingi hajui ikiwa mtu ambaye alitaka kumvutia kwa kuonekana kuwa mcha Mungu alivutiwa naye au la. Hata kama mtu huyo anavutiwa naye, na kumsifu nyuma ya mgongo wake, ni mara chache mtu husikia maneno katika sifa zake. Ingawa mtu anamsifu mbele yake, hii itasababisha uharibifu zaidi kwake. Niamini! Watu wakijua kwamba mtu fulani analia au anadhihirisha matendo yake ya ibada ili kujionyesha, watamchukia. Mtu huyu mwenye majigambo sasa atafakari ni kwa kiasi gani Allah عَزَّوَجَلَّ ambaye anajua kila kitu atamkasirikia!

*Aaj banta hoon mu'azziz jo khulay Hashr mayn 'ayb*
*Haye ruswa`ee ki aafat mayn phansoon ga Ya Rab*

*Tafsiri: Ninaonekana kuwa mtu mwema leo lakini nitafedheheka kabisa ikiwa makosa yangu yatafichuliwa Siku ya Hukumu. (Wasail-e-Bakhshish, uk. 91)*

## Matendo yataharibika

Hizi hapa ni baadhi ya Ayah na riwaya, zikifikisha da'awah njema, kwa nia ya kuongeza shauku kwa ajili ya kujiepusha na ubadhirifu na kuwaepusha wengine. Kwa hakika matendo yanayofanywa na watu wenye kujikweza wasio na hekima wanaopendelea maisha ya dunia kuliko maisha ya baada ya kifo hayatawanufaisha hata kidogo. Imenukuliwa hapa chini, katika muktadha huu, ni Ayah ya 15 ya Surah *Hood* pamoja na tafsiri yake kutoka ukurasa wa 418 na 419 wa Kanz-ul-Iman tukufu pamoja na Khaza`in-ul-'Irfan iliyochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji wa Dawat-e-Islami. Allah عَزَّوَجَلَّ amesema katika sehemu ya 12 ya Qurani Tukufu:

مَنْ كَانَ يُرِيْدُ الْحَيٰوةَ الدُّنْيَا وَ زِيْنَتَهَا

نُوَفِّ اِلَيْهِمْ اَعْمَالَهُمْ فِيْهَا وَهُمْ فِيْهَا لَا يُبْخَسُوْنَ ﴿١٥﴾

*Anaye taka maisha ya dunia na anasa zake, tutawapa malipo kamili ya vitendo vyao humo, wala hatutapunguza humo. [Kanz-ul-Iman (Tafsiri ya Quran)] (Sehemu ya 12, Surah Hood, Ayah 15)*

*(Akizungumzia Ayah hiyo hapo juu, Sayyiduna Ibn 'Abbas رَضِىَ اللّٰهُ عَنْهُمَا amesema, 'Wanaojivunia wanapewa malipo ya matendo yao mema ndani ya maisha yao ya kidunia, na hawadhulumiwi hata kidogo.'13).*

*Riya-kariyaun say bacha Ya Ilahi*
*Bana mujh ko mukhlis bana Ya Ilahi*

*Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ! Unilinde dhidi ya majivuno na unifanye mtumwa mwaminifu.*

## Tendo la kujistahi halikubaliki

Imeelezwa katika ukurasa wa 16 wa kitabu cha *'Riya Kari'* chenye kurasa 166, kilichochapishwa na Maktaba-tul-Madinah, idara ya uchapishaji ya Dawat-e-Islami: Rasuli Mpenzi na Mwenye Baraka صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَاٰلِهٖ وَسَلَّم amesema: Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ hakubali kitendo kilicho na unyago ndani yake sawa na punje ya haradali.' *( Attargheeb Wattarheeb, juzuu ya 1, uk. 36, Hadiyth 27)*

*Dikhaway sema mujh ko Ilahi bachana*
*Mujhay Apni rahmat say mukhlis banana*

*Tafsiri: Ewe Mwenyezi Mungu !عَزَّوَجَلَّ Niokoe na mambo ya kujifakhirisha na unibariki kuwa mnyoofu.*

## Pepo ni haramu kwa wanaojionyesha

Rasuli Mtukufu صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَالِهٖ وَسَلَّم amesema, 'Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ Ameitangaza Pepo kuwa ni Haraam kwa kila mtu mwenye kujionyesha. *( jam'- ul- Jawaami' lis Suyuti , juzuu 2 uk. 242 Hadithi 5329)*

Ndugu wapenzi wa Kiislamu! Anayeyaacha maisha haya kwa imani anaweza kusamehewa bila ya kuwajibika au kuingizwa Peponi baada ya kuadhibiwa kwa muda fulani, kutegemeana na mapenzi ya Mwenyezi Mungu. عَزَّوَجَلَّ Kwa hiyo, kutoa maoni kwa upande wa Hadiyth 'Pepo ni Haraam kwa mwenye kujionyesha' 'Allaamah Muhammad 'Abdur Ra`oof Manaawi رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema, 'Ina maana ya kuwa hataingia peponi mwanzoni. *(Fayd-ul-Qadeer lil-Manaawi, juzuu ya 2, uk. 286, Taht-al-Hadees 1725)*

*Khata`ayn mamiri 'afw Ghaffar ker day*
*Riya-kariyaun say Tu bayzar ker day*

*Tafsiri: Ewe Msamehevu! Tafadhali nisamehe makosa yangu na unifanye nishibishwe na majigambo.*

## Mfano wa kujionyesha

Akielezea kujionyesha kwa msaada wa mfano, Hujjat-ul-Islam, Sayyiduna Imamu Abu Haamid Muhammad bin Muhammad bin Muhammad Ghazali رَحْمَةُ اللّٰهِ عَلَيْه amesema: Mtu akisimama mbele ya mfalme, lakini lengo lake siku nzima ni kumtazama mja wake na si kupata ukaribu wa mfalme bali kumtazama mjakazi wake, hakika huku ni kumkosea heshima mfalme. Sasa fikiria! Ni kosa iliyoje na isiyopendeza kumwabudu Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ili kumvutia mja dhaifu na asiyejiweza ambaye hawezi kusababisha hasara wala faida! *(Ihya-ul-'Uloom, juzuu ya 3, uk. 369; muhtasari)*

*Ikhlas naykiyaun mayn ay Rab-e-Kareem day*
*'Day Aql-e-saleem mujhay qalb-e-saleem*

*Tafsiri: Ewe Mola wangu Mlezi* عَزَّوَجَلَّ ! *Nibariki kwa unyoofu katika matendo, pamoja na hekima kamilifu na moyo wa amani.*

## Ufafanuzi wa Riyaa [Kujionyesha]

Baada ya kupata ujuzi fulani juu ya uharibifu wa kujionyesha, hebu sasa tujifunze ufafanuzi wake. Ufafanuzi wa ubadhirifu wa madhambi ni kama ifuatavyo: "Kufanya ibada kwa nia yoyote isiyokuwa ya radhi ya Mwenyezi Mungu عَزَّوَجَلَّ ". Kwa maneno mengine, Riyaa ni kufanya ibada kwa nia ya kuwafahamisha watu kuhusu ibada ili mwenye kujionyesha apate pesa kutoka kwao au kusifiwa au kuchukuliwa kuwa mchamungu au kuheshimiwa nao. *(Az-Zawajir, juzuu ya 1, uk. 76)*

## Mifano 80 ya kujionyesha

(Ingawa mifano iliyotolewa hapa chini ni ya kujionyesha, maamuzi ya wengi wao yanaweza kubadilika kwa sababu ya tofauti ya nia.)

## Mifano 11 ya majigambo kuhusu Swalah

1. Kuswali mara kwa mara ili watu wamchukulie kuwa yeye ni thabiti sana katika Swalah.
2. Haafidh kuongoza Tarawiyh Swalah kwa ajili ya pesa.
3. Kuhudhuria Ijtima' ya Sunnah au kuswali pamoja na Jama'at au kufanya Sada-e-Madinah (yaani kuwaamsha Waislamu kwa Salat-ul-Fajr) siku ya ndoa ya mtu au wakati wa mazishi nyumbani kwa mtu. kwamba watu watamstaajabia na kumsifu wakisema sentensi kama 'Wah! Amefanya matendo mema hata katika tukio kama hilo!' (Hata hivyo, yeye hukosa matendo hayo kwa ukawaida katika siku nyinginezo).
4. Kuswali Swalah kwa utulivu na unyenyekevu wa mwili mbele ya watu ili kuwavutia.

5. Ikiwa mtu ambaye amehudhuria Ijtima'-e-Zikr-o-Na'at katika baadhi ya usiku mtukufu au ameswali Swala-ut-Tahajjud, anasugua macho yake au kunyoosha mchana mbele ya watu ili wapate kujua kuwa hakulala usiku bali amekesha akifanya matendo mema, hii ni dalili ya kujionyesha.

6. Kuswali [Swala ya Nafl kama vile] Ishraq, Chasht, Awwabeen na Tahajjud mbele ya watu ili wamchukulie kama mtekelezaji mzuri sana wa Swalah ya Nafl.

7. Iwapo mtu atachukuliwa kuwa ni mtekelezaji wa Tahajjud wa kawaida na mtekelezaji wa Nafl Siyam, ﴾صِيَام﴿ lakini kwa hakika, sivyo hivyo, kunaweza kuwa na hatari ya kujionyesha kwake. Kwa mfano, anapotambulishwa kwa watu kuwa ni mtendaji wa matendo haya mema, huinamisha kichwa chake na tabasamu usoni na kutoa hisia kana kwamba anafanya vitendo hivi. Ni mfano wa wazi wa kujionyesha.

8. Iwapo mtu ambaye ameamka kuswali Tahajjud anakohoa kwa sauti kubwa au kufanya mambo mengine ili mke wake au wanafamilia wengine waweze kuamka na kuvutiwa kumuona akiswali Tahajjud, ni mfano wa kujionyesha.

9. Kukaa Msikitini kwa muda mrefu baada ya kuswali ili watu wamchukulie kuwa ni mchamungu.

10. Kuswali mara kwa mara katika safu ya kwanza ya Masjid ili watu wamsifu na kuvutiwa naye.

11. Kuonyesha majuto mbele ya watu kwa kukosa safu ya kwanza au Jama'at ili watu wamchukulie kuwa ana shauku kubwa juu ya safu ya kwanza na Jama'at.

## Mifano 18 ya kujionyesha kwa wahubiri

1. Kutoa hotuba katika Ijtima' n.k ili watu waisifu hotuba yake na kumwita mhubiri mzuri.

2. Kusema sentensi za hisia kwa sauti kubwa ya kunguruma wakati wa hotuba au kukariri wanandoa kwa njia ya shauku ili hadhira waisifu hotuba hiyo kwa kumwita mhubiri mkubwa, kusema,b ﴾سُبْحٰنَ الله﴿ Marhaba n.k.

3. Kutumia sentensi za ajabu, maneno magumu, misemo ya Kiarabu wakati wa hotuba ili watu wamchukue kama mhubiri msomi na kuvutiwa naye.

4. Kusema sentensi kama hizo mwanzoni mwa hotuba kama vile: Nimekuwa nikisafiri kwa siku sita mfululizo; Ilinibidi nisafiri kwa saa 13 kabla sijafika hapa; Nimechoka sana, bado sijala chakula lakini nimekuja hapa kutoa hotuba n.k. Mhubiri anasema mambo kama hayo ili watu wamchukulie kuwa mhubiri mwaminifu anayejitolea mhanga katika njia ya Mwenyezi Mungu.

5. Kusema sentensi kama vile: Nimekuwa nikisafiri na Madani Qafilah kwa muda wa miezi 25; Mimi ni Waqf-e-Madinah (yaani mtu ambaye amejitolea maisha yake yote kwa shughuli za Madani); Nimekuwa nikitoa hotuba tangu siku ya kwanza kabisa; Nimekuwa nikihudhuria Madani Mashwarah kwa siku kadhaa, nimekuwa nikisafiri na Madani Qafilah mbili (au nne) kwa siku 3 kila mwezi. Kusema mambo haya kwa nia ya kupata heshima na sifa ili watu wamchukulie kuwa ni mhubiri bora anayejitolea mhanga kwa ajili ya Uislamu.

6. Kutoa Dars 50 au 100 kutoka kwa kitabu Faizan-e-Sunnat kwa siku pamoja na hisia ili watu wamthamini na kumsifu kwa jina la kutia moyo, na ili ndugu wakuu wa Kiislamu wa Dawat-e-Islami wampongeze na kumpa zawadi.

7. Kutoa hotuba kwa uzuri na ufasaha mbele ya mtu fulani mashuhuri au tajiri ili avutiwe na mhubiri na kumsifu.

8. Kuanzisha uhusiano na mwanasiasa fulani, waziri au mtu mashuhuri au tajiri ili watu watambue hilo au yeye mwenyewe atawaambia kwamba mwanasiasa fulani na kadhalika amevutiwa naye, anamwomba Du'a, kumbusu mkono au humtendea kwa heshima.

9. Kujaribu kumtia moyo mhudumu au afisa fulani kuja nyumbani kwa mhubiri ili watu wapate kujua kwamba maafisa wamevutiwa naye, na kuja nyumbani kwake kwa ajili ya Du’a au baraka.

10. Kumshauri afisa fulani au tajiri au kubainisha makosa yake, na kutoa hisia kwamba yeye (mhubiri) hashindwi hata na watu wenye ushawishi na wenye nguvu, na haoni woga katika kueleza amri ya Shari’ah mbele ya mtu yeyote.

11. Ikiwa mhubiri amewahi kumpa nasaha mtu tajiri na mashuhuri kufuga ndevu au akamshawishi mtu mashuhuri kutubia dhambi, kisha akataja tukio hili kwa ndugu wa Kiislamu au wakati wa hotuba yake ili watu wavutiwe naye, ni hivyo pia. dalili ya kujionyesha.

12. Kuweka macho chini, wakati wa kukaa na watu au kutoa hotuba au kufanya mazungumzo na wengine, ili watu waweze kuvutiwa naye, kwa kuzingatia kwamba anaweka macho yake chini kwa unyenyekevu na ameweka kufuli ya Madani kwenye macho yake (wakati macho yanazunguka na kutangatanga kila mahali asipokuwa na watu).

13. Kufanya mazoezi ya kuswali Swalah kwa utulivu na unyenyekevu au kuweka macho chini katika upweke ili aweze kufanya hivyo akiwa miongoni mwa watu, akiwavutia kwake. (Huku ni kujionyesha mara mbili kwa sababu kitendo kilichofanywa katika upweke halikuwa kwa ajili ya radhi ya Allah عَزَّوَجَلَّ bali ni kwa ajili ya kuwafanya watu wamuone kuwa ni mchamungu.)

14. Kujaza kijitabu cha Madani In'amaat anayefanya Fikr-e-Madinah mara kwa mara na kuwaambia wengine idadi ya Madani In'amaat mhubiri anafanya mazoezi ili watu wamsifu na kumtaja kama mfano kwa wengine, wakisema kuwa mhubiri fulani hutenda kwa uthabiti juu ya yote au mengi ya Madani In'amaat.

15. Kutumikia Uislamu, kusafiri na Madani Qafilah na kufanya juhudi za kidini zinazobeba tabu ili watu wamsifu mihanga aliyoitoa na watamhesabu kuwa ni mhubiri mwenye bidii na shauku.

16. Kusafiri katika nchi mbalimbali za ulimwengu katika njia ya Mwenyezi Mungu ili watu wasifu dhabihu alizozitoa, wamtaje kama mfano kwa wengine na kumwita mhubiri wa kimataifa.

17. Kulingania Sada-e-Madinah mara kwa mara, yaani kuwaamsha Waislamu kwa ajili ya Swala-ul-Fajr, ili watu wamsifu kwa kusema maneno kama vile: Haogopi giza na mbwa; wala baridi na mvua haziwezi kumzuia. Haijalishi anachelewa vipi kulala, hakosi Sada-e-Madinah.

18. Kufikisha da'awah njema kwa mtu au kumzuia na maovu ili watu wavutiwe na mhubiri na wamchukulie kuwa ni mtakiaji mkubwa wa Waislamu, huku akisema

sentensi kama vile: Ni mtu shupavu wa kidini na hawezi kubaki kimya akiona maovu. (Laiti mtu angeonyesha ujasiri huu wa kidini nyumbani kwake pia na kujaribu kuwa na fursa ya kuwarekebisha wanafamilia yake).

## Mifano 16 ya Riyaa kwa wasomaji na wasikilizaji wa Na’at

1. Kusoma Kurani Tukufu au Na’at katika Ijtima’ n.k ili watu wampe pesa, chakula na nguo; au wasifu sauti yake, namna ya kukariri, matamshi au michanganyiko.
2. Kujumuisha nakala nyingi kutoka kwa Hadaiq-e-Bakhshish n.k. katika Na’at inayosomwa ili watu wamsifu wakisema kwamba amejifunza idadi kubwa ya beti ngumu kwa moyo.
3. Kukariri Na’at kwa kumbukumbu bila kukiona kitabu ili watu wamsifu wakisema kwamba amejifunza Na’at nyingi sana kwa moyo.
